SUPA JACKPOT
TZS. 1,144,172,464
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#

SELECTED Superbrand Consumer & Industry Validated

**Maji** Kilimanjaro yashinda cheti cha ubora Super Brand

UKURASA 2


Nipashe TESA
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI
Itumie simu kulinda usalama nyumbani, vitega uchumi usibakie kuongea na 'Whatsap'

UKURASA 11


# Nipashe

Jumanne Agosti 15, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581403

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com 0745 700710 LIKE & FOLLOW US


# Wakili: Dk. Slaa yuko polisi tuhuma uhaini

• **Kina** Mwabukusi watinga Mahakama ya Rufani kesi ya Bandari... *Endelea ukurasa wa 2*

## YALIYOMO


UKURASA WA 4
**USAFIRISHAJI SAMPULI ZA KIBAIOLOJIA WAIPA TPC BIL. 2/- MWAKA MMOJA**
SHIRIKA la Posta Tanzania (TPC) limesema lilisafirisha zaidi ya sampuli 700,000 zikiwamo...

UKURASA WA 4
**SHULE ZA SEKONDARI DAR KUWA ZA BWENI**
MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamilla, amesema wana mpango wa...

UKURASA WA 8
**'VIJANA WENGI HAWANA ELIMU KUJIKINGA NA VVU'**
UKOSEFU wa elimu sahihi kwa vijana jinsi ya kujikinga na maambukizi mapya ya Virusi vya Ukimwi (VVU), umetajwa sababu ya vijana...


## Anayedaiwa kuzikwa mwaka 2018 aibuka, afunguka alikokuwa

UKURASA 3




Meneja Mradi wa Kampuni ya Superbrands, Jawad Jaffer (kushoto), akimkabidhi tuzo ya Superbrand Mkuu wa Idara ya Mauzo na Masoko wa Kampuni ya Bonite Bottlers Ltd, Christopher Loiruk, kutokana na maji ya Kilimanjaro kuwa bidhaa bora kwa kinywaji kisicho na kilevi wakati wa utoaji wa tuzo hizo jijini Dar es Salaam jana.
**PICHA: JUMANNE JUMA**

NUSU YA MADAKTARI KUFELI

# Serikali yaunda kamati kuchunguza

UK. 18

**MICHEZO** YANGA YAMFUNGUA MACHO ROBERTINHO UK.24

**KATUNI** UK.6

# Wakili: Dk. Slaa yuko polisi tuhuma uhaini

**Na Mwandishi Wetu**

ALIYEKUWA Balozi wa Tanzania Sweden, Dk. Wilbroad Slaa anayedaiwa kukamatwa na Jeshi la Polisi juzi, kufanyiwa upekuzi na kufikishwa Kituo cha Polisi Osterbay, anatarajiwa kufikishwa mahakamani wakati wowote kuanzia sasa kwa tuhuma za uhaini, wakili wake amedai.

Wakili wa Balozi Dk. Slaa, Dickson Matata, aliiambia Nipashe jana kuwa muda wa saa 24 zinazoruhusiwa kisheria kwa mtu kushikiliwa polisi zilikuwa hazijafika tangu kukamatwa, hivyo kwa muda huo asingehoji chochote kwa jeshi hilo.

Alidai kuwa walichoambiwa na polisi ni kwamba mteja wake huyo atafikishwa mahakamani leo au kesho kwa mashtaka ya uhaini.

"Tumefika kituoni, tumemwona na kuhakikisha kwamba anapata huduma zote za kibinadamu na kwa kuwa bado hazijatimia saa 24 zinazotakiwa kisheria kwa mtu kukaa ndani kabla ya kupelekwa mahakamani, tunasubiri tuone itakuwaje.

"Lakini tumeambiwa atafikishwa mahakamani kesho (leo) au keshokutwa (kesho). Tunaendelea kufuatilia," alisema Wakili Matata.

Juzi, wakili huyo alitoa taarifa kupitia mitandao ya kijamii kwamba Balozi Dk. Slaa alikuwa amekamatwa na alikuwa anahojiwa kwa tuhuma za uchochezi, lakini baadaye tuhuma zilibadilishwa na kuwa za uhaini.

Wakili huyo alidai Balozi Dk. Slaa anaendelea vyema kiafya na amepatiwa huduma zote muhimu ikiwamo chakula na nguo za kuzuia baridi kama inavyotakiwa kwa mujibu wa sheria.

Balozi Dk. Slaa anadaiwa kukamatwa na Jeshi la Polisi nyumbani kwake Mbweni mkoani Dar es Salaam juzi mchana na baadaye kufanyiwa upekuzi.

Kwa mujibu wa Wakili Matata, mbali na kushikiliwa, polisi pia walichukua vifaa vyake vya kielektroniki ikiwamo simu yake ya mkononi, kompyuta mpakato na flash mbili.

Wadau mbalimbali na washirika wa karibu wa Dk. Slaa, akiwamo Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu na Askofu Bandekile Mwamakula wa Kanisa la Moravian la Uamsho Tanzania, wamezungumzia kukamatwa kwa balozi huyo aliyewahi kuwa Katibu Mkuu wa CHADEMA, wakikosoa kukamatwa kwake wakidai ni mpango wa kunyamazisha wanaokosoa suala la uwekezaji wa Bandari.

Wakati hali ikiwa hivyo kwa Balozi Slaa, Wakili Boniface Mwabukusi na Mdude Nyagali ambao pia walikamatwa kwa makosa ya aina hiyo, hawajafikishwa mahakamani licha ya kupita muda wa saa 24 tangu wakamatwe.

Msemaji wa Jeshi la Polisi, David Misime, alipotafutwa na Nipashe jana kueleza kuhusu hatima ya Balozi Slaa na wenzake, hakupokea simu na pia hakujibu ujumbe mfupi wa maandishi aliotumiwa.

Juzi, Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, alipoulizwa alisema; "Kama kuna taarifa hiyo, tutawaambia si huwa tunawaita? Basi tutawapatia. Lakini hadi sasa hakuna taarifa yoyote kutoka ndani ya jeshi".

## Maji Kilimanjaro yashinda cheti Super Brand

**Na Maulid Mmbaga**

MAJI ya kunywa ya Kilimanjaro yanayozalishwa na Kampuni ya Coca-Cola yameingia kwenye orodha ya vinywaji bora na kutunukiwa cheti cha 'Super Brand' baada ya utafiti uliofanywa na Super Brand Afrika Mashariki, kwenye kundi la vinywaji visivyokuwa na kilevi.

Bidhaa hiyo ya Bonite Bottlers Limited inaungana na wanachama wengine wawili wa IPP gazeti la Guardian na ITV ambao wameshinda nembo hiyo mara kwa mara.

Akizungumza katika hafla ya utoaji wa tuzo hizo jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa mradi wa Super Brand Afrika Mashariki, Jawad Jaffer, alisema maji ya Kilimanjaro yana sifa ya kutambuliwa katika kitengo cha vinywaji visivyo na kilevi kutokana na utafiti wa watumiaji, huku akiwataka washindi kudumisha ubora unaowawezesha kutambuliwa.

"Kupanda juu ni rahisi, lakini kukaa kileleni si rahisi; inahitaji kujituma, kufanya kazi kwa bidii, kutegemewa na uadilifu," alisema Jaffer.

Baada ya kupokea cheti hicho, Mkuu wa Kitengo cha Mauzo na Masoko wa Bonite Bottlers, Christopher Loiruk, alisema mafanikio hayo yametokana na chanzo cha kipekee cha bidhaa hiyo mjini Moshi, mkoani Kilimanjaro.

"Pia ni kwa sababu ya viwango vya ubora ambavyo tunazingatia ambavyo vimewekwa nchini na kimataifa na vile vile uongozi thabiti na wafanyakazi wenye weledi wa hali ya juu," alisema.

Kampuni nyingine zilizokabidhiwa vyeti vya ubora wa juu ni Dar Ceramica Centre, (GSM), Benki ya NMB na Shirika la Bima la Taifa (NIC), ambayo ni kampuni pekee ya serikali iliyoingia kwenye orodha hiyo.

Mkurugenzi Mkuu wa NIC, Dk. Elirehema Doriye, alisema ina maana kubwa kwa kampuni inayomilikiwa na serikali kusimama katika sekta yenye ushindani mkubwa kama vile bima.



Mafundi wakiendelea na ujenzi wa kivuko kipya cha Ijinga-Kahangala kinachojengwa katika karakana ya Songoro Marine iliyoko Ilemela mkoani Mwanza, kimegharimu Sh. bilioni 5.2 kitakapokamilika kitatoa huduma Ijinga na Kahangala wilayani Magu mkoani Mwanza. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

SAKATA LA BANDARI

# Kina Mwabukusi watinga Mahakama ya Rufani

**Na Kulwa Mzee**

JOPO la mawakili linalowakilisha walalamikaji wanne katika kesi ya kupinga Mkataba wa Ushirikiano wa Kiuchumi na Kijamii kati ya Tanzania na Dubai (IGA) wa Bandari iliyotupiliwa mbali na Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya wiki iliyopita, limewasilisha kusudio la kuukatia rufani uamuzi huo katika Mahakama ya Rufani.

Hatua hiyo imekuja siku chache baada ya Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya kutupilia mbali kesi hiyo Agosti 10 mwaka huu kutokana na ilichokisema kuwa mkataba haujakiuka vifungu vya katiba.

Wakili Philipo Mwakilima, kwa niaba ya mawakili wenzake Mpale Mpoki, Boniface Mwabukusi na Livino Ngalimitumba, waliwasilisha kusudio hilo jana katika Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya.

Mwakilima alisema kuwa baada ya kuwasilisha kusudio hilo, wanasubiri mwenendo wa shauri hilo uandaliwe wapewe kwa ajili ya kuwasilisha rufani yao wakiwa na sababu mbalimbali za kupinga uamuzi.

Mahakama katika uamuzi wake ilisema mkataba huo unaolenga kuendesha, kuwekeza na kuendeleza bandari nchini, haukukiuka vifungu vya katiba, hivyo shauri halina mashiko. Linatupiliwa mbali.

Hukumu hiyo ilitolewa na jopo la majaji watatu; Jaji Dunstan Ndunguru ambaye ni kiongozi wa jopo, Jaji Mustafa Ismail na Jaji Abdi Kagomba.

Mwenyekiti wa Jopo, Jaji Ndunguru alisema mkataba huo ulitiwa saini Oktoba 25, 2022 na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa kwa niaba ya Serikali ya Tanzania, baada ya kupewa nguvu ya kisheria na Rais Samia Suluhu Hassan, huku Katibu Mkuu wa Wizara hiyo akishuhudia.

Alisema watu wanne walionyesha dosari kubwa katika mkataba huo na katika hati ya madai waliwasilisha misingi minne ya malalamiko yao.

Hata hivyo, jopo hilo la majaji lilisema hakukuwa na dosari za kisheria kufanya mkataba wa IGA kuwa batili.

Shauri hilo lilifunguliwa na wanasheria watatu kutoka mikoa tofauti, Alphonce Lusako, Emmanuel Chengula, Raphael Ngonde na Mwananchi Frank Nyalus dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na Katibu wa Bunge la Tanzania, ambaye ni mtendaji mkuu na mratibu wa shughuli za Bunge.

Walalamikaji wanawakilishwa na Mawakili Mpale Mpoki, Boniface Mwabukusi, Livino Ngalimitumba na Philipo Mwakilima.

Wajibu maombi wanawakilishwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Mark Mlwambo, Wakili Mkuu wa Serikali, Edson Mweyunge na Wakili wa Serikali, Stanley Kalokola.


Walalamikaji katika shauri hilo wanapinga makubaliano yanayohusisha uwekezaji katika Bandari za Tanzania zilizoko katika mwambao wa bahari na katika maziwa, kuwa ni batili kwa kuwa yana ibara zinazokiuka sheria na Katiba ya nchi.

Wanadai makubaliano hayo yanahatarisha mamlaka ya nchi na usalama wa taifa na kwamba yaliridhiwa na Bunge kinyume cha utaratibu bila kuwapa nafasi ya kutosha wananchi kutoa maoni yao.

Kesi hiyo ilianza kusikilizwa Julai 25 mpaka Julai 28 na hukumu kutolewa Agosti 10 mwaka huu.

**HABARI KITAIFA**

# Anayedaiwa kufariki dunia na kuonekana, azungumza



Mwashi Lutema, anayedaiwa kufariki dunia miaka mitano iliyopita. **PICHA: NEEMA HUSSEIN**

**Na Neema Hussein,** MLELE

KATIKA hali isiyo ya kawaida mtu mmoja aliyetambulika kwa jina la Mwashi Lutema (33), aliyefariki dunia miaka mitano iliyopita, inadaiwa ameonekana akiwa hai katika Kijiji cha Kamalampaka, Wilaya ya Mlele, mkoani Katavi.

Tukio hilo limezua taharuki kwa watu wengi wakiwamo ndugu wa mwanamke huyo wakidai ndugu yao alifariki dunia Aprili 2018 baada ya kusumbuliwa na maradhi ya kifua kwa muda mrefu.

Akizungumza na Nipashe, shemeji wa mwanamke huyo, Elias Maduhu, alisema kabla ya kifo chake alikuwa akiugua homa na alipozidiwa walimpeleka kwa mganga wa kienyeji kwa ajili ya matibabu, lakini bila mafanikio alifariki dunia.

"Baada ya kufariki tulifanya mazishi, lakini kabla ya kufariki alikua akiishi na mume wake katika Kijiji cha Songambele kwa muda wa miaka miwili na walikuwa hawajapata mtoto.

"Tukio la kuonekana akiwa hai nilisikia baada ya kupigiwa simu na kwenda kushuhudia na kweli nikakuta ni mwenyewe, mwanzo sikuamini ila nilipomuona kwa sura na kuongea naye, ndipo nilipoamini.

Alikuwa kwenye ofisi za Mtendaji wa Kata ya Kamalampaka, waliniambia ametokea Mpanda maeneo yasiyojulikana," alisimulia shemeji huyo.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kamsisi, Leonard Nkomo, alisema taarifa hizo alizipata akiwa kwenye kikao cha Mkuu wa wilaya kuwa kuna mtu amepatikana baada ya kupotea kwa muda wa miaka mitano.

"Tukaanza kuulizana huyo mtu alikua amepotea au alienda wapi? Ndiyo wakasema kuwa alikuwa amefariki dunia ameonekana Kijiji cha Kamalampaka, nilivyofika kijijini ikabidi nimpigie afande mmoja anaitwa Omary, akasema yuko eneo langu amemleta huyu mtu alikuwa amefariki dunia, basi nikamwambia ngoja nije nijiridhishe kama ni mwananchi wangu nimuone na mimi.

"Ikabidi nitoke nyumbani niende nikashuhudie mimi mwenyewe na nikamtafuta Mwenyekiti wa Kitongoji cha Ilelanda alikofariki mwanamke huyo, akasema ni kweli kabisa alifariki miaka mitano aliyopita na nguo aliyozikwa nayo ni hii. Ikabidi nimtafute mzee mwingine mwenyeji wa kitongoji hiki naye akasema ni kweli mtu huyo alifariki."

Mwenyekiti huyo alisema tukio hilo halijawahi kutokea na wananchi wamelipokea kwa mshangao mkubwa huku kila mtu akitaka kumuona mwanamke huyo.

Nipashe ilizungumza na mwanamke anayedaiwa kufariki dunia ambaye na kusema anachokumbuka ni kuwa kuna watu walimchukua, wengine akiwaona anawakumbuka wengine hawakumbuki na kwamba walivaa mavazi yenye rangi nyeusi, nyekundu na nyeupe.

Alisimulia kuwa baada ya kumchukua walimpeleka sehemu isiyojulikana, lakini alirudi mwenyewe kutafuta ndugu zake baada ya kuwakimbia watu hao waliomchukua wakiwamo wanawake, wanaume, vijana wa kike na kiume pamoja na wazee.

"Huko nilikuwa naishi mazingira magumu, nilikuwa nakula vitu ambavyo havieleweki nakula mchanga, sabuni na matope, mara wanibake wamenitesa sana wamenipiga, wakaniumiza ila hawajanifanyisha kazi yoyote ngumu zaidi ya kunitesa, kunipiga, kunilisha mchanga na vingine vichafu," alisema Mwasi.

Diwani wa Kata ya Kamsisi, Leonard Kiyungi, alisema tukio hilo ni la kwanza kutokea na yeye kulishuhudia. Alisema taarifa hizo alizipata kutoka kwa wananchi na baada ya kufuatilia alibaini mtu huyo ni mkazi wa Kijiji cha Songambele, Kata ya Kamsisi na alikuwa akiishi Kitongoji cha Ilelanda.

Alisema alipopata taarifa hizo alienda kujiridhisha, lakini alipofika nyumbani kwa anayedaiwa kufariki na kuonekana, aliambiwa mhusika amepelekwa kwa kaka yake.

Alisema tukio hilo halijawahi kutokea kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Mlele.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**KAZI, VIJANA, AJIRA, NA WENYE ULEMAVU**

**TAARIFA KWA UMMA**
**WITO KWA VYUO NA TAASISI ZA MAFUNZO KUSHIRIKIANA NA SERIKALI KUTOA MAFUNZO YA UANAGENZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024**

1.0. Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu inatekeleza Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi. Maeneo makuu ya utekelezaji wa Programu hii ni: Mafunzo ya Uanagenzi; Mafunzo ya kuendeleza ujuzi kwa Wafanyakazi; Mafunzo ya Uzoefu wa kazi wahitimu wa vyuo; na Kurasimisha Ujuzi uliopatikana nje ya mfumo rasmi wa Mafunzo. Lengo la mafunzo ni kuipatia nguvukazi ya Taifa hasa vijana ujuzi wa kuwawezesha kushindana katika soko la ajira ndani na nje ya nchi na hatimaye kuongeza wigo wa kujiajiri au kuajiriwa.

2.0. Katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Ofisi ya Waziri Mkuu imepanga kutoa mafunzo ya Uanagenzi kwa Vijana 4,500 katika Fani mbalimbali. Miongoni mwa mafunzo yatakayotolewa ni Ubunifu wa Mitindo na Ushonaji Nguo, Ufundi Bomba, Uashi, Useremala, Uchomeleaji na Uungaji vyuma, Upakaji rangi na maandishi ya alama, Utengenezaji wa vipuri vya mitambo, Ufundi Magari na Mitambo, umeme wa majumbani na viwandani, TEHAMA, Umeme wa Magari, Huduma za Hoteli na Utalii, Ukataji madini ya vito, na Kilimo.

3.0. Mafunzo yatatolewa kwa vijana wa kitanzania wenye umri usiozidi miaka 35 na yatakuwa ya muda wa miezi Sita (6) chuoni na miezi miwili mahala pa kazi. Mafunzo yatafanyika katika mikoa yote nchini.

4.0. Sifa za Vyuo na Taasisi kushiriki kutoa Mafunzo:
   a) Vyuo vilivyosajiliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) yenye Daraja A, B na C;
   b) Vyuo na taasisi zenye uwezo na kutoa mafunzo kwa fani husika kuanzia wanafunzi 100 na kuendelea;
   c) Vyuo vyenya Wakufunzi walioajiriwa na chuo husika na wanatambulika na Serikali;
   d) Vyuo vyenye uwezo wa miundombinu ya kufundishia kozi husika; na
   e) Vyuo vyenye uzoefu usiopungua miaka mitano (5) na vimetoa mafunzo husika mfululizo.

5.0. Vyuo vyenye sifa za kutoa Mafunzo ya uanagenzi vinashauriwa kuwasilisha maombi husika kwa utaratibu ufuatao:-
   a) Barua ya kuomba kutoa mafunzo ikianisha fani zitakazotolewa na idadi ya wanafunzi kwa kila fani;
   b) Sifa za wakufunzi watakaotoa mafunzo (Wasifu wa watoa mafunzo CV);
   c) Cheti cha usajili wa chuo;
   d) Cheti cha Mlipa Kodi (Tax Identification Number); na
   e) Maelezo mengine ya ziada kadiri itakavyofaa.

6.0. Vyuo na Taasisi zitakazowasilisha maombi zitafanyiwa upekuzi kuona kama zina uwezo wa kutoa mafunzo husika. Vyuo na Taasisi zitakazokidhi vigezo zitaitwa kwa majadiliano na Serikali kuhusu namna bora ya kushirikiana kutoa mafunzo husika.

7.0. Vyuo na Taasisi zinazopenda kushiriki kutoa mafunzo viwasilishe maombi kwa Katibu wa Bodi ya Ununuzi, Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, **S. L. P. 2890, DODOMA, Mji wa Serikali, Mtumba, Mtaa wa Kazi.** Maombi yawasilishwe kabla ya tarehe 28 Agosti, 2023 saa 9.00 Alasiri.

**Imetolewa na:**
**KATIBU MKUU**



Meneja Mkuu wa Chama Kikuu cha Ushirika wa Wakulima Masasi-Mtwara na Nanyumbu (MAMCU),Biadia Matipa, akisoma bei za mauzo ya zao la mbaazi kwenye mnada wa kwanza wa zao hilo tangu lilipoingia kwenye mfumo wa stakabadhi ghalani uliofanyika jana Kijiji cha Mkululu wilayani Masasi, bei ya juu ilikuwa Sh.2,003 na chini Sh.1,950. **PICHA: HAMISI NASRI**

# Usafirishaji sampuli za kibaiolojia waipa TPC bil. 2/- mwaka mmoja

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Posta Tanzania (TPC) limesema lilisafirisha zaidi ya sampuli 700,000 zikiwamo za kibaiolojia nchini.

Kwa kusafirisha sampuli hizo, shirika hilo liliingiza Sh. bilioni mbili, zikilipwa na serikali kupitia Wizara ya Afya na washirika wa maendeleo.

Macrice Mbodo, Postamasta Mkuu, alibainisha hayo jana alipozungumza na wahariri wa vyombo vya habari wakati wa semina iliyoandaliwa kwa ajili ya kundi hilo.

"Hii ni huduma na anayesafirisha zile sampuli ni serikali. Tumepata zaidi ya Sh. bilioni mbili kwa mwaka uliopita.

"Unajua siku zote huwa tunasema kuna taasisi za serikali na binafsi, lakini kwa kifupi huwa kuna taasisi zingine tunazisahau zinaitwa taasisi za nchi. Zenyewe zinatekeleza majukumu ya nchi," alifafanua.

Alisema kuwa usafirishaji wa sampuli hizo unafanywa na shirika hilo baada ya kuingia makubaliano na serikali kufanya kazi hiyo.

Alisema kazi hiyo wakati mwingine inahusisha sampuli hatarishi zikiwamo za magonjwa kama vile Ebola, Virusi vya Ukimwi, kansa, kifua kikuu (TB), kipindipindu na UVIKO-19. Hivyo, ni usafirishaji unaofanywa kwa umakini mkubwa, pia usiri.

Katika semina hiyo, Mbodo pia alisisitiza mkakati wao wa kutanua huduma za Posta nchini, akisema wamepanga wawe na wakala kila kijiji.

Alitaja mafanikio ya shirika yanajumuisha kuongeza mapato yake, kutoa huduma kidigitali, limenunua mitambo ya kisasa ya ukaguzi na kusafirisha vifaa vya (vishikwambi) Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022.

Vilevile, alisema kuwa shirika sasa lina magari yake, yakiwamo mabasi yanayobeba abiria na kusafirisha vipeto katika mikoa mbalimbali nchini huku likishirikiana vyema na Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) katika usafirishaji.

"Tumeimarisha mtandao wa usafirishaji ili kuhakikisha tunakidhi vionjo vya wateja wetu, na wananchi kwa ujumla, kwa mwaka huu ulioisha, tumeongeza magari mengine 14. Sasa tuna vyombo vya moto zaidi ya 300 kwa nchi nzima.

"Pia, tumeingia mikataba ya usafirishaji na kampuni mbalimbali za meli kwa ajili ya usafirishaji madini, kampuni mbalimbali za ndege. Kwahiyo, tunakwenda nchi zote duniani, lengo ni kuhakikisha mwananchi anapata fursa ya kuhudumiwa na mtoa huduma za Posta wa mamlaka aliyopewa," alisema.

Kiongozi huyo pia alisema wamewezeshwa na Umoja wa Posta Duniani kwa ajili ya kutengeneza mfumo wa utumaji na upokeaji fedha ndani na nje ya nchi kwa njia ya kielektroniki.

**WENYE ULEMAVU**

Postamasta Mkuu huyo pia lisema changamoto ya elimu kwa baadhi ya watanzania ni sababu ya kundi la watu wasioona na viziwi kushindwa kunufaika na fursa zinazotolewa katika shirika hilo ya kusafirishiwa vifurushi vyao bila kutozwa gharama.

Alisema, kundi hilo linalindwa kwa kuzingatia sheria iliyotungwa na Umoja wa Posta Duniani. Baadhi ya watanzania hawajui fursa hiyo ndiyo maana kundi hilo limekuwa likipambana kusafirisha mizigo yake kwa njia ya usafiri wa mabasi.

"Kwa miongozo ya Umoja wa Posta Duniani, viziwi na walemavu wa macho wanatakiwa kusafirisha vitu vyao bure na asitozwe chochote lakini hapa kwetu baadhi ya watu hawana uelewa na kusababisha viziwi na wasioona wasinufaike na fursa hii," alisema.

Alisema mfumo unaopaswa kutumiwa na kundi hilo likitaka kusafirisha mzigo kwa mfumo huo ni kwenda ofisi hizo na kujitambulisha na watapewa huduma hiyo kwa kusafirishiwa mizigo yao bila kutozwa gharama yoyote.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri (TEF), Deodatus Balile, alipongeza Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa kuandaa utaratibu wa mashirika yaliyo chini yake, kuwa na vikao na wahariri na waandishi wa habari kueleza utekelezaji wa shughuli zao.

Alisema utaratibu huo unapaswa kufanywa na wizara, akidokeza kuwa kuna mawaziri wanakwepa kuzungumza na waandishi wa habari "kwa kuwa utendaji wao una walakini".

## Shule za sekondari Dar kuwa za bweni

**Na Mary Geofrey**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamilla, amesema wana mpango wa kuzifanya shule za kutwa za kidato cha kwanza hadi cha nne kuwa za bweni ili kuwaepusha wanafunzi na mazingira hatarishi, vikiwamo vitendo vya ukatili.

Chalamila aliyasema hayo jana katika Shule ya Sekondari ya Wavulana Azania wakati Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angellah Kairuki akikabidhi magari 10 kwa ajili ya maofisa elimu sekondari wa halmashauri nane nchini kwa lengo la kuongeza ufanisi, usimamizi na ufuatiliaji wa elimu nchini.

Alisema lengo la kuzifanya shule za sekondari za mkoa huo kuwa za bweni ni kuwawezesha wanafunzi kusoma kwa bidii na kuongeza ufaulu wao.

Alisema hatua hiyo inafuatia tathimini ya ufaulu ya mkoa huo kuonyesha shule za kitado cha tano na sita ambazo ni za bweni zinafanya vyema katika matokeo ya kitaifa tofauti na shule za kidato cha nne.

"Shule hizi zitatusaidia kusimamia wanafunzi katika makuzi yao, muda wanaofika shuleni, walimu kuwa na muda wa kuwaongoza vyema. Na hili andiko tutakuletea mezani kwako Mheshimiwa Waziri ili hata kama kuna ufadhili, wautazame kwa jicho la tofauti mkoa wetu," alisema.

Chalamila alibainisha mkoa huo una shule za sekondari 455 zikiwamo za serikali 182 na za watu binafsi 273. Alitolea mfano Shule ya Wavulana Azania ambayo ni ya bweni, matokeo ya kitado cha sita yanaonyesha wamepata daraja la kwanza hadi la tatu na hakuna daraja la nne wala sifuri.

Naye, Waziri Kairuki aliwataka maofisa elimu kutumia vyema magari hayo kwa ajili ya kurahisisha shughuli za elimu nchini katika kuongeza ubunifu wa utekelezaji wa majukumu yao.

Alisema magari yalikabidhiwa katika halmashauri za Hai, Mtama, Songea Manispaa, Bukoba Vijijini, Monduli, Handeni, Ikungi na Sumbawanga Manispaa na magari mengine mawili yamepelekwa TAMISEMI kwa ajili ya usimamizi wa shughuli za elimu.

Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Dk. Charles Msonde, alisema serikali imeamua kununua magari kwa ajili ya kuwezesha watendaji wa shule za msingi na sekondari kutekeleza majukumu yao kikamilifu.

Alisema serikali imetoa Sh. bilioni 20.6 kwa ajili ya kununua magari 200 yakiwamo 184 kwa ajili ya maofisa elimu sekondari kusaidia kurahisisha shughuli zao na 16 kuwa makao makuu ya taasisi mbalimbali za TAMISEMI.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Anna Henga, alilieleza Nipashe jana kuwa mpango huo una manufaa makubwa kwa wanafunzi wa mkoa huo wenye watu zaidi ya wakazi milioni 5.4 kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022.

"Itasaidia sana kwani kwa mujibu wa utafiti wetu (LHRC), vishawishi vingi watoto huvipata njiani," alisema Henga.

Mzazi wa wanafunzi watatu wa sekondari, James Mlawa alisema ni ndoto ya wazazi kusomesha watoto wao shule za bweni, ili kuwanusuru na matatizo na purukushani za mitaani, lakini wengi hawana vipato.

"Kama serikali imeona umuhimu wa wanafunzi wa sekondari hususani wa Dar es Salaam kukaa bwenini, litakuwa jambo la msingi sana na watakuwa wapo kwenye usalama kuliko huku mitaani," alisema.

Mzazi mwingine, Mariam Yusuph ana mtazamo kuwa watoto wakiishi bwenini, familia zitataabika kwa sababu watoto wanategemewa kusaidia familia majukumu ya nyumbani.

"Kuna wengine wakirudi shuleni inabidi waingie kwenye biashara. Kama watakuwa bwenini itakuwa faida kwa wanafunzi kuwasaidia kufaulu ila wazazi watakosa usaidizi," alisema.



CHAMA CHA WALIMU TANZANIA (CWT)

# KUITWA KWENYE USAILI

Katibu Mkuu wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) anawatangazia wote walioomba nafasi ya kukitumikia chama cha Walimu Tanzania (CWT) kwa nafasi za Katibu wa CWT Wilaya pamoja na Mkuu wa Idara ya Walimu wenye Ulemavu kuwa usaili utafanyika mnamo tarehe 19 Agosti 2023, kuanzia saa mbili kamili asubuhi katika ukumbi wa St. Gasper Hotel Jijini Dodoma.

**MUHIMU.**

1. Kila msailiwa aje na vyeti halisi vya kitaaluma na kitaalamu pamoja na cheti cha kuzaliwa.
2. Kila msailiwa afike na hati ya mshahara (salary slip) za mwezi Juni, na Julai 2023.
3. Gharama za usafiri, chakula na malazi zitakuwa juu ya msailiwa.

Imetolewa na:

**Maganga M. Japhet**
**KATIBU MKUU - CWT**

| S/N | JINA | WILAYA |
|---|---|---|
| 1. | ABDALLAH K. MAGONGO | S.L.P ILALA -DAR ES SALAAM |
| 2. | ABDALLAH M. CHAMBA | S.L.P NYAMAGANA -MWANZA |
| 3. | ADRIAN MWEMEZI PROSPER | S.L.P MEATU - SIMIYU |
| 4. | AGREY S. MHINZA | S.L.P NZEGA- TABORA |
| 5. | AISHA SUDI KAYUMBA | S.L.P BAHI -DODOMA |
| 6. | ALEX LUKANIZYA | S.L.P BARIADI TC -SIMIYU |
| 7. | ALLY ATHUMANI | S.L.P BAHI -DODOMA |
| 8. | ALLY R. MKETO | S.L.P KALIUA – TABORA |
| 9. | ALOYS L. THOMAS | SL.P MISENYI- KAGERA |
| 10. | ANACLET P. BABWELATA | S.L.P BUKOBA |
| 11. | ANNA MBAWALA | S.L.P NAMTUMBO - RUVUMA |
| 12. | ARISTIDES D. ISHENGOMA | S.L.P ILEMELA -MWANZA |
| 13. | BARAKA A. SANGA | S.L.P TANGANYIKA-KATAVI |
| 14. | BEATRICE F. MJEMA | S.L.P MUSOMA MC- MARA |
| 15. | CECILIA BATAMALE SEBASTIAN | S.L.P MULEBA-KAGERA |
| 16. | CHAMWEZI G. CHAMWEZI | S.L.P KALAMBO- RUKWA |
| 17. | CHARLES B. KIKOTI | S.L.P KALAMBO -RUKWA |
| 18. | CHARLES W. CHACHA | S.L.P 263 KARATU -ARUSHA |
| 19. | CLEMENCE JOEL SUKUM | S.L.P BABATI- MANYARA |
| 20. | CLEMENT MAHEMBA | S.L.P CHAMWINO- DODOMA |
| 21. | DANSTAN PRIVA MELLA | S.L.P MOSHI DC -KILIMANJARO |
| 22. | DARABU M. GANAKU | S.L.P NYAMAGANA- MWANZA |
| 23. | DAUDI ENOCK DAUD | S.L.P ELEMELA KAGERA |
| 24. | DAUDI MPOLE | S.L.P SINGIDA- SINGIDA |
| 25. | DAVID W. PHARLES | S.L.P BAGAMOYO- PWANI |
| 26. | DORICE S. MLANGWA | S.L.P KIBAHA -PWANI |
| 27. | DOTTO J. KIHONGO | S.L.P NJOMBE -NJOMBE |
| 28. | DOTTO MSANJILA | S.L.P KIGOMA - KIGOMA |
| 29. | DUNIA G. LUVENA | S.L.P TEMEKE -DAR ES SALAAM |
| 30. | DUWE VITALI ANDREA | S.L.P KARATU- ARUSHA |
| 31. | EBENEZER ERICK SHAO | S.L.P ROMBO -KILIMANJARO |
| 32. | EDINA DAUDI | S.L.P SINGIDA MC -SINGIDA |
| 33. | ELIAS KAYAGAMBE BOAZ | S.L.P BUHIGWE-KIGOMA |
| 34. | ELIDAD I. MATHAYO | S.L.P MOROGORO- MOROGORO |
| 35. | ELIFADHILI JULIASI LUDOVIC | S.L.P MISUNGWI-MWANZA |
| 36. | ELIWIRIAM MIRISHO NNKO | S.L.P SIHA- KILIMANJARO |
| 37. | EMMANUEL M. DAVID | S.L.P S/WANGA M-C -RUKWA |
| 38. | EMMANUEL PATRICK JOHN | S.L.P ILALA -DAR ES SALAAM |
| 39. | ENOCK SIMWINGA | S.L.P MPANDA -KATAVI |
| 40. | ERICK BEBWA | S.L.P ITILIMA -SIMIYU |
| 41. | EURITHA SAMSONI SHILAGA | S.L.P KAHAMA -SHINYANGA |
| 42. | FAIDHA HASSANI NYAMBUKA | S.L.P MANYONI- SINGIDA |
| 43. | FESTO BARUSHA STANSLAUS | S.L.P SHINYANGA DC -SHINYANGA |
| 44. | FORTUNATA F. MUYAGA | S.L.P TABORA MC -TABORA |
| 45. | FRANSISCA JACKOBO | S.L.P IKUNGI -SINGIDA |
| 46. | FRIDA ANTONY MALLEY | S.L.P BABATI -MANYARA |
| 47. | FRIDA N. MWIWULA | S.L.P IRINGA -IRINGA |
| 48. | GABRIEL STEPHANO GWALTU | S.L.P SINGIDA DC -SINGIDA |
| 49. | GASPAR O JAKA | S.L.P MOROGORO MC -MOROGORO |
| 50. | GEORGE RASHID GAILANGA | S.L.P KISHAPU- SHINYANGA |
| 51. | GEORGE SALVATORY YAPESA | S.L.P MONDULI- ARUSHA |
| 52. | GERALD I. MGAYA | S.L.P NJOMBE - NJOMBE |
| 53. | GERVAS A. SANGA | S.L.P MAKETE -NJOMBE |
| 54. | GRACE MUTAENGERWA | S.L.P SERENGETI -MARA |
| 55. | HADIJA O. RUMAMBO | S.L.P NYAMAGANA -MWANZA |
| 56. | HALPHA S. MFANGA | S.L.P BABATI -MANYARA |
| 57. | HAMISI SHABANI MTUNDUA | S.L.P SINGIDA MC -SINGIDA |
| 58. | HANCE MWALYEKO | S.L.P RUKWA |
| 59. | HASHIMU S. NTANDU | S.L.P IKUNGI -SINGIDA |
| 60. | HASSAN ABDALLAH KIRIBA | S.L.P 20 MISUNGWI -MWANZA |
| 61. | IBRAHIM M. STANSLAUS | S.L.P TARIME-MARA |
| 62. | IVONA J. BAJUMUZI | S.L.P BUKOBA – KAGERA |
| 63. | JACOB SARME NAWE | S.L.P LIWALE-LINDI |
| 64. | JAMES MZIGABA BULEGE | S.L.P 6005 MKINGA -TANGA |
| 65. | JANE MTINDYA | S.L.P KILOSA -MOROGORO |
| 66. | JAPHARY RAMADHAN OMARY | S.L.P SHINYANGA DCSHINYANGA |
| 67. | JOB MUVUNYI GAHANGA | S.L.P CHAMWINO- DODOMA |
| 68. | JOHN JOSEPH LUKIKO | S.L.P BUKOMBE -GEITA |
| 69. | JOHN NTUGWA MAKONGOLO | S.L.P KAHAMA SHINYANGA |
| 70. | JOHN SEBASTIANI | S.L.P MKALAMA-SINGIDA |
| 71. | JOYCE KIMARIO CLEMENCE | S.L.P GEITA TC - GEITA |
| 72. | JULIAN BRUNO KAYOZA | S.L.P DODOMA |
| 73. | JUMA NGASOMA SAWAKA | S.L.P TEMEKE- DAR ES SALAAM |
| 74. | JUMA ABDALAH DEDU | S.L.P NGARA -KAGERA |
| 75. | JUMANNE MTIPA | S.L.P BABATI- MANYARA |
| 76. | JUSTUS RICHARD KAGYA | S.L.P SHINYANGA MC - SHINYANGA |
| 77. | KISHERI KIBORA | S.L.P ILEMELA-MWANZA |
| 78. | LUCAS TITO ZACHARIA | S.L.P MISSENYI K-AGERA |
| 79. | MAGAMBO J. PETRO | S.L.P BARIADI -SIMIYU |
| 80. | MATHIAS WILOMO | S.L.P MPANDA-KATAVI |
| 81. | MATHIASI NYAKWAKE | S.L.P CHAMWINO -DODOMA |
| 82. | MAYALA C. LUSAWI | S.L.P SERENGETI -MARA |
| 83. | MAYUNGA JITINYA | S.L.P MTWARA MC- MTWARA |
| 84. | MBAGA M. IDI | S.L.P TANGA JIJI -TANGA |
| 85. | MBOYI E. KIDENDEI | S.L.P BUTIAMA- MMARA |
| 86. | MONICA JOHN MATIKO | S.L.P TEMEKE -DAR ES SALAAM |
| 87. | MULUNGU JAILOSI MSAFIRI | S.L.P ILEJE -SONGWE |
| 88. | MUSSA H. MPOTA | S.L.P IRINGA DC-IRINGA |
| 89. | MWAKALINGA A. LUPAKISYO | S.L.P KILINDI- TANGA |
| 90. | MWASONI JUMANNE MADINA | S.L.P SONGWE-SONGWE |
| 91. | MWINYI SALIM MWINYI | S.L.P MBOZI- SONGWE |
| 92. | NICHOLAUS TUBONEYE | S.L.P 73 TUNDUMA-SONGWE |
| 93. | NOLASCO P. MUGALULA | S.L.P SONGEA V-RUVUMA |
| 94. | OMARI HALIFA SAID | S.L.P KILWA-LINDI |
| 95. | OSCAR NSOLO | S.L.P BARIADI-SIMIYU |
| 96. | PACIENCE C. MPONDA | S.L.P KISARAWE- PWANI |
| 97. | PASKALI DIONISI TSAFU | S.L.P MBULU -MANYARA |
| 98. | PASKALI KAKAY AMMO | S.L.P BABATI - MANYARA |
| 99. | PAUL DEOGRATIAS MSENJI | S.L.P KASULU -KIGOMA |
| 100. | PETEONILA S. GADIYE | S.L.P MANYARA |
| 101. | PETER S. LUSAMBO | S.L.P NKASI -RUKWA |
| 102. | PHELISIAS KUBYULA | S.L.P ILEMELA- MWANZA |
| 103. | PHILEMON PETER KISININI | S.L.P IRINGA |
| 104. | PRISCA B. MGALULA | S.L.P DODOMA JIJI -DODOMA |
| 105. | PROSPER KADEWELE | S.L.P DODOMA |
| 106. | RAHEL B. CLEMENT | S.L.P MASWA -SIMIYU |
| 107. | RAHEL MANDAGO SYLVESTER | S.L.P MEATU -SIMIYU |
| 108. | RAMADHAN SAID MPONDOKA | S.L.P TEMEKE -DAR ES SALAAM |
| 109. | RAMADHANI IDDI KABELWA | S.L.P IKUNGI SINGIDA |
| 110. | RAYMOND YOTHAMU LUTEMBA | S.L.P MSALALA/KAHAMA- SHINYANGA |
| 111. | REHEMA HASHIM KAZIRI | S.L.P ARUMERU-ARUSHA |
| 112. | RICHARD N. SHAGUNGU | S.L.P KILOSA-MOROGORO |
| 113. | ROBERT BUNDALA | S.L.P KIBAHA-PWANI |
| 114. | RUTH W. MLEMBA | S.L.P IRINGA |
| 115. | SAIDA FADHILI OMARI | S.L.P KISARAWE -PWANI |
| 116. | SARA SELEMANI ABDALAH | S.L.P MASASI -MTWARA |
| 117. | SELEMAN B. MALINGISHI | S.L.P GEITA DC- GEITA |
| 118. | SHABAN YUSUFU YUSUFU | S.L.P MTWARA V -MTWARA |
| 119. | SHIDA R. OTWOMA | S.L.P MUSOMA MC -MARA |
| 120. | SHUARY SEIF CHEMBERA | S.L.P CHEMBA -DODOMA |
| 121. | SITTA LADISLAUS SILAS | S.L.P BUKOBA – KAGERA |
| 122. | SOPHIA MAKARIUS | S.L.P SONGEA MC RUVUMA |
| 123. | TATU A. KINGWALA | S.L.P CHALINZE - PWANI |
| 124. | THADEI PAUL MUSHI | S.L.P 27 HAI - KILIMANJARO |
| 125. | THECLA MBIKI | S.L.P MOROGORO MC-MOROGORO |
| 126. | THOBIAS MUSIMU MGANGA | S.L.P BIHARAMULO-KAGERA |
| 127. | THOMAS MADODI COSTER | S.L.P KIGOMA DC- KIGOMA |
| 128. | TOSHA SHOMARI | S.L.P SONGEA MC- RUVUMA |
| 129. | TUPA AMANI MBWAMBO | S.L.P TABORA MC- TABORA |
| 130. | TUZO SALEHE MOHAMED | S.L.P UBUNGO- DAR ES SALAAM |
| 131. | VALENTINE K. MGONDA | S.L.P URAMBO-TABORA |
| 132. | VEDASTUS JOSEPH RUGANGILA | S.L.P KAHAMA - SHINYANGA |
| 133. | WCLIFFE OMBORI | S.L.P IGUNGA -TABORA |
| 134. | YEREMIAH G. KITWANGE | S.L.P NAMTUMBO- RUVUMA |
| 135. | ZAINA FADHILI MNDEME | S.L.P KILWA - LINDI |

## ORODHA YA WAOMBAJI NAFASI YA MKUU WA IDARA YA WALIMU WENYE ULEMAVU

| S/N | JINA LA MWOMBAJI | WILAYA/MKOA |
|---|---|---|
| 1. | ACHIENG ROBBY ODAMO | S.L.P MUSOMA |
| 2. | ALOYCE MASERO JOSEPHAT | S.L.P MAGU |
| 3. | BAETRICE MOHAMED MOSHI | S.L.P ARUSHA |
| 4. | BENENDICT D. MSERI | S.L.P DAR ES SALAAM |
| 5. | BENENDICT HILOLIMUS MWINGIRA | S.L.P TEMEKE |
| 6. | BENJAMIN ASTON MTAMBO | S.L.P UYUI |
| 7. | BENJAMIN K. MAYENGELA | S.L.P SINGIDA |
| 8. | BONIFACE ZACHARIA NAALY | S.L.P KASULU |
| 9. | CONSOLATA MUTALEMWA MULOKOZI | S.L.P DAR ES SALAAM |
| 10. | DINA A. MALISA | S.L.P MWANZA |
| 11. | EDWINA P. GWAMAKOMBE | S.L.P MOROGORO |
| 12. | ELIWAJA JACOB MSUKUMA | S.L.P MOROGORO |
| 13. | EMMANUEL RICHARD MPONGO | S.L.P MONDULI |
| 14. | GABRIEL JEROME SHIRIMA | S.L.P ARUSHA |
| 15. | GILBERT ROBERT | S.L.P KYERWA |
| 16. | GORDON ROBERT MWAKALUKWA | S.L.P MOROGORO |
| 17. | JACOB F. CHAWALA | S.L.P MWANZA |
| 18. | JAPHARI R. OMARY | S.L.P KISHAPU |
| 19. | JAMES MZIGABA BULEGE | S.L.P MKINGA |
| 20. | JOVITUS JOSEPH MUHANDIKI | S.L.P UYUI |
| 21. | MATUKU MARCO MUGETA | S.L.P UKEREWE |
| 22. | MWITA LADISLAUS MAGIGE | S.L.P KIBAHA |
| 23. | NGOMERO HAMISI | S.L.P PANGANI |
| 24. | NZELA CHARLES JAGADI | S.L.P KALIUA |
| 25. | PIUS MORICE KAZIBURE | S.L.P NANYUMBU |
| 26. | PROSPER KADEWELE | S.L.P DODOMA |
| 27. | ROBERT BUNDALA | S.L.P KIBAHA - PWANI |
| 28. | ROBERT MANASE KILASI | S.L.P SUMBAWANGA |
| 29. | SALOME AUBREY KISSIMBO | S.L.P ROMBO |
| 30. | SELEMAN K. IDRISSA | S.L.P BUKOBA |
| 31. | SILAS MASUI MAGUNGUMA | S.L.P MVOMERO |
| 32. | SILVANUS SHIJA SULU | S.L.P TABORA |
| 33. | SINGILA KASUMUNI | S.L.P IRINGA |
| 34. | SONGALAEL P. MIGIRE | S.L.P KITETO |
| 35. | STEPHANIA STEPHENE NGONYANI | S.L.P IRINGA |
| 36. | STEPHEN S.N MUTABUZI | S.L.P KYERWA |
| 37. | WAHID RASHID SALAMI | S.L.P HANDENI |

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wamachinga wasitengwe ugawaji vibanda Mwenge

**WAKATI** serikali ilipoamua kubadilisha eneo lililokuwa stendi ya daladala Mwenge, Wilaya ya Kinondoni jijini Dar es Salaam na kuwa sehemu itakapojengwa Machinga Complex, wafanyabiashara wadogo waliahidiwa kupewa kipaumbele wakati jengo hilo litakapokamilika kwa kupewa vibanda vya kufanyia biashara zao.

Wafanyabiashara hao walitengewa eneo lingine la kufanyia biashara zao ambalo ni barabara ya kuelekea kiwanda cha Coca-Cola, eneo hilohilo la Mwenge, wakati wakisubiri jengo lao kukamilika.

Baadhi yao waliendelea kuuza bidhaa zao kwa kupanga chini wakati wa jioni na wengine kwa kupanga kwenye meza.

Wengine walihamia eneo la Makumbusho ambalo sasa ndiyo kituo kikuu cha mabasi ya daladala.

Wafanyabiashara wadogo wamedai wanaona dalili ya kutengwa kupewa vibanda hivyo na badala yake nafasi kubwa inapewa wafanyabiashara wakubwa, jambo wanalodai ni kinyume cha makubaliano ya awali wakati ujenzi unaanza mwaka 2018.

Wafanyabiashara hao walikumbusha kuwa mwaka wa fedha 2018/19, serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Kinondoni, iliwaomba kupisha ujenzi wa mradi wa kituo cha magari katika eneo hilo na kuwaahidi kupewa kipaumbele kupata majengo ya biashara mradi ukikamilika.

Kwa sasa ukipita eneo la Mwenge utaona mabadiliko makubwa mandhari yake ni ya kupendeza, jengo la vibanda vya biashara limeleta mwonekano mpya na wa kuvutia.

Ukipita wakati wa usiku jengo hilo linapendeza zaidi kwa jinsi taa zinavyopendezesha jengo hilo na kuonekana eneo jipya zaidi.

Basi mwonekano huo usibadili lengo lililowekwa tangu wakati jengo hilo likipangwa kujengwa kwamba kipaumbele kitakuwa kwa wafanyabiashara waliokuwa eneo hilo tangu mwanzo.

Barua ya Halmashauri ya Kinondoni katika baadhi ya vipengele inaeleza wazi kuwa "unatakiwa kupisha mradi wa ujenzi na baada ya kukamilika utatakiwa kufika na barua hii Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni ili uweze kukabidhiwa eneo lako la biashara."

Ahadi hiyo pia ilisisitizwa na Waziri Mkuu, Aprili mwaka jana alipokwenda kukagua maendeleo ya mradi huo.

Hata hivyo, wafanyabiashara hao wameshangazwa baada ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, alipokwenda kukagua mradi huo akiwa ameongozana na uongozi wa halmashauri mwezi Julai, kujulishwa kuwa barua walizopewa zenye taarifa ya kupewa kipaumbele ni za kisiasa, hivyo wanatakiwa kufuata utaratibu wa kuomba nafasi pamoja na wafanyabiashara wengine.

Kauli ya Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Manispaa ya Kinondoni, ilieleza kuwa manispaa imebadilisha utaratibu wa upangishaji wa vibanda vyake na sasa unafanyika kwa njia ya mnada.


Mpango huo ni maelekezo ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa halmashauri zote nchini na uliridhiwa na vikao vya madiwani na kutangazwa kupitia vyombo vya habari, mwezi Mei, mwaka huu.

Imeelezwa kuwa lengo la utaratibu huo mpya ni kuwapa nafasi sawa wafanyabiashara wote nchini wenye nia ya kukodisha vibanda hivyo na kuondoa malalamiko ya upendeleo na mazingira ya rushwa.

Majibu hayo yanatoa ufafanuzi wa malalamiko kutoka kwa wafanyabiashara hao, lakini wahenga walisema ahadi ni deni. Kama waliahidiwa kupewa kipaumbele na uwezo wa kulipia vibanda wanao, wasikilizwe ili kuondoa malalamiko.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Tuzitafakari mara mbili hekaheka za mgambo na machinga D'Salaam

Na Nasra Sereri, UDOM

**HALI** ya wafanyabiashara wa mitumba katika eneo la Mwenge Sokoni, Dar es Salaam yazidi kuwa mbaya, kutokana na msuguano wao na askari mgambo wanaowakataza kufanya biashara maeneo wanayopanga na kuuza vitu vyao.

Lengo la mgambo kuwafukuza ni kuwahamishia eneo jingine, ambalo serikali imewapangia wakauze huko bila gharama zozote, kwa madai yao wafanyabiashara hao wanachafua mazingira na wanaongeza msongamano wa watu kwenye barabara bila sababu ya msingi.

Lakini, inaonekana baadhi ya wamachinga hao wamekuwa wagumu kuondoka katika eneo hilo la Mwenge, kwa sababu hapo ndiko wanakoamini kuna wateja zaidi, kuliko pale walikotengewa na serikali, kwamba biashara haziendi kwa kukosa wateja.

Serikali imeshawapa maeneo mbalimbali Wamachinga ndani Dar es Salaam, ambako mojawapo ni karibia na iliko kiwanda cha Cocacola, Mikocheni. Katika eneo hilo, serikali haitawatoza kodi ya malipo kutunza mizigo yao.

Nilipozungumza na baadhi ya wafanya biashara hao walisema kuwa mgambo wanavyofanya vurugu za kuwafukuza huwa wanaharibu mali zao na vile vile huwaingizia hasara sana.

Wanaumizwa sana kitendo cha kurushiwa mabomu ya machozi na wanateseka sana, vile vile wanaomba serikali ingewaacha mahali ambapo wateja wao wamepazoea.

Nilipojaribu kuwauliza Wamachinga hao, mahali ambako ni mbadala wa soko kwa maana ya jirani nala Cocacola, baadhi wanasema kwamba wako tayari kuondoka kwa muda, ila pale ujenzi wa stendi mpya ya Mwenge utakapokamilika wanaomba wahamie ndani ya stendi wakauze bidhaa zao humo.

Kwa upande mwingine, nilizungumza na wafanyabiashara ambao wana maduka mahali hapo, wanaonaje suala la wamachinga kufukuzwa kwa maeneo ya karibu hapo, na kupelekwa huko Mikocheni, wengine wakasema sio vizuri na kwamba hakuna cha maana wanachokizuia kwa kubaki Mwenge, bali ni wanatafuta tu pesa.

Hapo wakafafanua kwamba kuhusu suala la usafi wa mazingira, wakihoji mbona wengi hufanya usafi wakiwa wanafunga mizigo yao na vilevile, mahali wanakopanga bidhaa zao?

Hapo wanena kwamba sio sehemu ambayo magari mengi hupita kama njia, bali ni sehemu magari husimamisha na kuegesha kwa muda ili kuingia maofisini au madukani basi.

Wapo waliofafanua kwamba, serikali haina makosa kuwafukuza eneo hilo, kwa sababu walishaambiwa wasipange tena bidhaa zao mahali hapo, kwani wameshatafutiwa sehemu mbadala, lakini hawasikii na wameendelea kukiuka sheria, hivyo basi ndo maana mgambo wao wanafanya kazi yao.

Mengi yameongelewa na wafanyabiashara wa Mwenge Sokoni, lakini hatima ipo mikononi mwa serikali na uamuzi wao wenyewe, kwani wakisema waendelee kubaki mahali hapo, itakuwa hasara, kwa sababu kila kukicha watasumbuliwa hadi waondoke.

Pia anataja wanapoamua kuondoka na kufuata msimamo wa serikali, basi huo ndio utakuwa mwisho wa vurugu hizo, vilevile utakuwa mwisho wa mzozo kati yao na migambo.

Wamachinga hofu yao kubwa ni kuhamia eneo jipya, watakosa wateja, lakini swali linaibuka kama mtu ana bidhaa nzuri, si lazima wateja watakuja tu?

Pia hakuna asiyejua kwamba, wamehamishwa eneo la biashara na kwa sasa wapo karibia na kiwanda cha Cocacola. Vilevile eneo hilo sio mbali sana na walipo mwanzo, hivyo basi sio vigumu watu kutokuja kabisa ukizingatia maeneo yale yamezungukwa na ofisi, chuo, makazi ya watu na kiwanda, hata kufanya isiwe rahisi kupata wateja wapya katika eneo hilo.

Wamachinga wamedumu kuwa watu muhimu sana kwa Watanzania, kwani huuza bidhaa mbalimbali kwa bei ya chini, ambao Watanzania wengi wanaweza kununua.

Vilevile, soko la Mwenge limezoeleka kwa Wamachinga wengi wanaouza bidhaa hasa za mitumba, hali inayochangia Imani sio rahisi kwao kuhama na wana - Dar es Salaam wasiwatafute kupata bidhaa wanazohitaji .

Katika mustakabali wa maelewano, ni busara mgambo wakatafuta mbadala wa kuwahamisha katika maeneo waliyokatazwa, kwa njia wanazotumia sasa zinaleta msuguano, ambao unatabia ya kukaribisha mabaya na magumu.



Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza Tanzania, Mzee Ramadhani Nyamka (kushoto), akipokea ripoti kuhusu afya ya akili magerezani katika ofisi ndogo ya Kamishna Jenerali wa jeshi hilo iliyopo Ukonga, Dar es Salaam kutoka kwa Prof. Joseph Mbatia, ambaye ni kiongozi wa utafiti uliofanywa na Asasi ya Afya ya Akili Tanzania (MEHATA) kwa kushirikiana na wataalamu wa Jeshi la Magereza. **PICHA: JESHI LA MAGEREZA**

# Mkutano jukwaa la viongozi taasisi za umma waiva

**Na Jenifer Gilla**

MSAJILI wa Hazina, Nehemia Mchechu, anatarajiwa kukutana na Jukwaa la Viongozi wa Taasisi za Umma, Agosti 19 hadi 21, mwaka huu, katika mkutano utakaofanyika mkoani Arusha ambao mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Rais Samia Suluhu Hassan.

Akizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, Mchechu, alisema katika mkutano huo kutafanyika mambo makuu matano, ikiwamo kujadili changamoto za kiuendeshaji zinazokabili taasisi hizo katika utekelezaji wa majukumu yao.

Alisema pia watapitia kwa pamoja na kukumbushana mambo muhimu ambayo wenyeviti na watendaji wa taasisi hizo wanapaswa kuyazingatia katika usimamizi wa utendaji wao wa kazi.

Vilevile, alisema watapitia kwa pamoja maboresho ya usimamizi wa taasisi pamoja na vigezo vipya vya utendaji kazi vitakavyotolewa na Ofisi ya Msajili wa Hazina.

Alisema pia viongozi hao watapata mafunzo ya uongozi, ili kuboresha utendaji kazi wao pamoja na kujadili na kupitia dira ya maendeleo ya taifa ya mwaka 2050.

Aidha, alisema kutakuwa na tuzo za kuzitambua taasisi zinazofanya kazi nzuri zilizowekwa katika makundi manne ambazo zitatolewa na Rais Samia.

Mchechu alisema lengo la mkutano huo ni kutengeneza taasisi zenye ufanisi mzuri ili ziongeze faida au kuchangia katika magawio yao kwenye serikali na zile zinazotegemea kulipwa mshahara za serikali hadi leo ziachane na suala hilo.

Mwenyekiti wa jukwaa hilo, Sababa Moshingi, alisema mkutano huo ni muhimu kwa kuwa utawakutanisha viongozi na wenyeviti wa taasisi hizo kujadili mambo yatakayosaidia taasisi zao kuchangia ipasavyo katika ukuaji wa uchumi wa nchi hiyo.

Makamu Mwenyekiti wa jukwaa hilo, Latifa Hamisi, alisema lengo la jukwaa hilo ni kurahisisha mawasiliano ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu yao.

"Napenda kutoa wito kwa viongozi wenzangu wote kuendelea kushiriki pamoja na kuunga mkono mawazo mbalimbali ya kuendeleza taasisi zetu na taifa ili tuende sambamba na mabadiliko ya dunia," alisema Latifa.

# Zambia yaonyesha nia ushirikiano Hospitali rufani Mbeya

**Na Mwandishi Wetu**

HOSPITALI ya Taifa ya Zambia imeonyesha nia ya ushirikiano na Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya katika utoaji wa huduma bora za afya kwa wananchi wa Zambia kwa lengo la kubadilishana uzoefu na ujuzi.

Akizungumza baada ya kikao cha pamoja uongozi wa Hospitali ya Taifa ya Zambia, Dk. Lazaro Mboma, mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji wa MZRH, alisema lengo la ziara hiyo ni kushirikishana utaalamu katika utoaji wa matibabu bora na sahihi kwa wananchi na ukuzaji wa teknolojia ya TEHAMA katika kuimarisha upatikanaji wa kumbukumbu sahihi za matibabu kwa mfumo wa e-Medical ikiwa ni pamoja na tiba mtandao ili kurahisisha utendaji kazi na kuongeza ufanisi ikiwamo kukuza uhusiano wa muda mrefu kati ya watoa huduma za afya.

"Tunapenda kuushukuru uongozi wa Hospitali ya Taifa ya Lusaka Zambia kwa kutupokea na kutupa fursa ya kubadilishana uzoefu katika nyanja mbalimbali za matibabu na huduma bora za afya. Tunaamini kuwa ziara hii itasaidia kuboresha huduma za afya zetu na kuleta mabadiliko chanya katika sekta ya afya nchini zetu," alisema Dk. Mboma.

Alisema kuwa ushirikiano huo unajumuisha kutoa huduma za matibabu kwa wagonjwa kutoka nchi zote mbili wanaohitaji matibabu maalum ambayo hayapatikani katika hospitali zao za ndani, vilevile kubadilishana wataalamu wa afya kati ya hospitali zote mbili kupitia programu za mafunzo mtambuka ya kubadilishana wataalamu.

Naye Dk. Musaku Mwenechanya, Mganga Mkuu Mfawidhi wa Hospitali ya Taifa ya watoto Zambia, alisema hospitali hiyo inatarajia kuwa ushirikiano huo utaleta manufaa makubwa kwa hospitali zote mbili na kuimarisha huduma za afya kwa wananchi wa nchi hizo na wako tayari kupokea wataalamu wao na kuendelea kushirikiana kwa karibu katika siku zijazo.


"Tuna furaha ya kuanzisha ushirikiano huu na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya mpango huu utatuwezesha kutumia nguvu na rasilimali za kila taasisi ili kunufaisha jamii tunazohudumia," alisema.

Naye Balozi wa Tanzania nchini Zambia, Luteni Jenerali Mathew Edward Mkingule, alipongeza hatua zilizofikiwa kwa hospitali zote mbili katika ufanikisha ushirikiano huo kuwa mataifa yote mawili yana uhusiano mkubwa baina ya nchi kwa miaka mingi kupitia waasisi wake na ana imani kuwa ushirikiano huo utaimarisha zaidi uhusiano huo na kutazamia kubadilishana mbinu bora katika utoaji na usimamizi wa huduma za afya.

Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya hutangaza tiba utalii (Medical Tourism) kitaifa na kimataifa na inatoa huduma za kibingwa na vipimo mbalimbali zikiwamo huduma za upasuaji wa kibingwa kama upasuaji wa moyo, ubongo na uti wa mgongo, figo, ini na matibabu ya saratani, huduma za magonjwa ya akili na matibabu ya kisaikolojia, magonjwa ya wanawake kama matibabu ya uzazi, huduma za upasuaji wa mifupa na mishipa ya damu, magonjwa ya kisukari na figo.

## KABWELA

**Na Fadhil Mohammed**



# Mfumo stakabadhi ghalani wainua soko la mbaazi

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

JUMLA ya kilo 2,092,595.00 za mbaazi za wakulima wa Chama Kikuu cha Ushirika wa Wakulima Masasi, Mtwara na Nanyumbu (MAMCU), zimeuzwa katika mnada wa kwanza wa zao hilo tangu serikali ilipotangaza rasmi kuingia kwenye mfumo wa stakabadhi mazao ghalani kama ilivyo kwa korosho na ufuta.

Mnada wa mbaazi umefanyika jana katika kijiji cha Mkululu, Halmashauri ya Wilaya ya Masasi na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali wa mazao wakiwamo wafanyabiashara kutoka ndani na nje ya nchi na bei ya juu ya mnada imeuzwa kwa Sh. 2003 huku ya chini ikiwa ni Sh. 1,950.

Akizungumza mbele ya wakulima baada ya kumalizika mnada huo, Meneja Mkuu wa MAMCU, Biadia Matipa, alisema kwa mara ya kwanza chama hicho kufanya mnada wa mbaazi tangu serikali ilipoagiza zao hilo kuuzwa kwa mfumo wa stakabadhi mazao ghalani.

Matipa alisema wakulima wamekuwa na mwamko chanya wa kupeleka mbaazi zao ghalani kwa ajili ya kuitikia agizo hilo la serikali la kuuzwa kwa mfumo wa stakabadhi ghalani mfumo ambao unatija kwa wakulima na kuondokana na kunyonywa na wafanyabiashara.

Alisema MAMCU inatarajia kufanya minada sita ya mbaazi kwa msimu huu kwa bei ya juu Sh. 2003 na ya chini Sh. 1,950.

Mwenyeikiti wa wakulima wa chama hicho cha Masasi, Siraji Mtenguka, alisema kwa vile zao hilo limeshaanza kuuzwa kwa mfumo wa stakabadhi ghalani wakulima wanapaswa kuepuka kuuza zao hilo kwa mfumo ambao sio rasmi ili wasije kunyonywa na wafanyabiashara.

Baadhi ya wakulima waliosiriki kwenye mnada huo, wameipongeza serikali kwa kusimamia bei nzuri ya zao hilo ambayo imeandika historia kuingizwa kwenye mfumo rasmi wa stakabadhi mazao ghalani.

Jamila Hassani, mkulima wa mbaazi wa kijiji cha Mkululu alisema wanaishukuru serikali kwa kuingiza zao hilo kwenye mfumo wa stakabadhi mazao ghalani na kwamba umewainua wakulima wa zao hilo.

Alisema kuwa awali wakulima walikuwa wakiuza kwa Sh. 200 hadi 800.



Makamu Mwenyekiti wa UWT Taifa, Zainab Shomari, akionyesha mfano wa ufyatuaji matofali yanayotumika kwenye ujenzi wa miundombinu ya maji (tangi) katika Kijiji cha Malaja Kata ya Nkalakala wilayani Mkalama mkoani Singida. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Vijana wengi hawana elimu kujikinga VVU'

**Na Halfani Chusi**

UKOSEFU wa elimu sahihi kwa vijana jinsi ya kujikinga na maambukizi mapya ya Virusi vya Ukimwi (VVU), umetajwa sababu ya vijana wengi kupata maambukizi hayo.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Watu Wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (NACOPHA), Deogratius Rutatwa, wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Rutatwa aliwaalika wadau kushiriki mdahalo wa kitaifa wa kujenga ubia kati ya wadau na jamii, kuweka mkakati endelevu kupambana na maambukizi hayo kufikia malengo ya kitaifa na kimataifa ya vifo 0.3 ifikapo 2030.

Alisema vijana wengi wanapata maambukizi hayo kwa kutokujua njia za kujikinga pamoja na kutotumia kinga (kondomu) wakati wa tendo la kujamiiana.

"Serikali kupitia Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu ilisema maendeleo ya watu wanaoishi na maambukizi hayo wanajua imefikia asilimia 96, walioko kwenye matibabu asilimia 98, waliofubaza asilimia 97, haya ni matokeo makubwa ambayo Watanzania tunapaswa kuyalinda.

"Kazi hii sio ndogo, inahitaji juhudi za kimkakati wa pamoja kati ya NACOPHA, Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania TACAIDS, na Ofisi ya Waziri Mkuu tumekubaliana kutengeneza mkakati wa kitaifa utakao tokana na mjadala wa kitaifa ambao kilele chake utakuwa Septemba," alisema Rutatwa.

Alisema wataweka mkakati kuonyesha Tanzania imelenga kutokomeza janga hilo na kuendelea kuunga mkono juhudi za serikali katika mapambano hayo, huku akiyataka mashirika mbalimbali kuendelea kuwaunga mkono ili kufanikisha mpango huo.

Ofisa Uraghbishi TACAIDS, Jumanne Issango, alilipongeza baraza hilo kwa kuisaidia serikali kupambana na ugonjwa huo, akiwataka wadau mbalimbali kujitokeza kwa wingi kwenye mjadala huo kupata maoni ya pamoja ili kusukuma juhudi hizo.

# Serikali yatoa zaidi ya mil. 300/- kujenga madarasa

**Na James Mwanamyoto**

SERIKALI imetoa Sh. milioni 331 kupitia mradi wa BOOST kujenga madarasa ili kutatua tatizo la msongamano wa wanafunzi Shule ya Msingi Mambamba 'B' wilayani Tandahimba.

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Deogratius Ndejembi, alisema fedha hizo zimetolewa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Ndejembi alisema hayo katika Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba, baada ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa kumpatia fursa ya kuzungumza na wakazi wa eneo hilo.

Alifafanua kuwa, Rais Suluhu alitafuta zaidi ya bilioni 230 kwa ajili ya kujenga shule mpya na madarasa nchi nzima kupitia Mradi wa BOOST kwenye maeneo ambayo shule zina msongamano wa wanafunzi au kukosekana shule na Tandahimba imenufaika na ujenzi wa Shule ya Msingi ya Mambamba 'B' iliyogharimu Sh. milioni 331.

"Mhe. Waziri Mkuu milioni 331 imejenga madarasa haya mazuri yenye kupendeza katika Shule hii ya Msingi ya Mambamba 'B' ambayo yatasaidia kutatua changamoto ya msongamano wa wanafunzi uliopo katika shule mama ya Mambamba, ikiwa ni pamoja na kuwaondolea adha wanafunzi kutembea umbali mrefu," alisema.

Pia, alisema Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba imepokea Sh. milioni 95 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za walimu wa shule ya msingi na milioni 95 nyingine kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za walimu wa shule za sekondari.

Kadhalika, Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) imetenga fedha kwa ajili ya kukarabati barabara ya kilomita 7.2 ya kutoka Mambamba kwenda Mwimbi hadi Tandahimba ili iweze kupitika katika majira yote.



**Mhe. Waziri Mkuu milioni 331 imejenga madarasa haya mazuri yenye kupendeza katika Shule hii ya Msingi ya Mambamba 'B' ambayo yatasaidia kutatua changamoto ya msongamano wa wanafunzi.**





## Madiwani wapiga marufuku fedha za walimu kwenda CWT

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Karatu, mkoani Arusha, wameridhia ombi la walimu zaidi ya 500 kutokatwa mishahara yao na Chama cha Walimu Tanzania (CWT), baada ya waalimu hao kujitoa kwenye chama hicho na kujiunga na chama cha CHAKUHAWATA.

Akiwasilisha ombi hilo jana katika baraza la madiwani wilayani humo, Katibu Msaidizi wa chama hicho, Deogratius Mmao alilaani kitendo cha idara ya utumishi kuendelea kuwakata mishahara yao na kuelekeza CWT.

Mmao alisema kuwa walimu hao wamefuata taratibu zote za utumishi na kujiunga na CHAKUHAWATA.

"Tunaomba uamuzi wa kujiunga na chama kipya uheshimiwe na siyo kuendelea kuwakata mishahara yao na kuendelea kuipeleka CWT ambako wamejitoa na kwa kuendelea kupeleka michango yao huko, ni kutengeneza mgogoro mwingine," alisema.

Wakichangia hoja hiyo, madiwani hao waliunga mkono hoja na kumtaka Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Juma Hokororo kupitia idara ya utumishi, kuheshimu hoja ya walimu hao na kuacha kuwakata mishahara na kuelekeza CWT, badala yake waelekeze kwenye chama kipya.

Hivyo, walimwagiza mkurugenzi huyo kupitia idara ya utumishi kuanzia Agosti mwaka huu kuhakikisha hakuna mshahara wa mwalimu unaokatwa na chama hicho ili kuheshimu uhuru wa mwalimu.

Naye Mwenyekiti Msaidizi wa CHAKUHAWATA, Festo Mbilinyi alishukuru baraza la madiwani kwa kupokea ombi lao, aliomba mchakato huo uharakishwe, ili uweze kuingia kwenye utekelezaji.

Alisema: "Hili limetuumiza kichwa kwa muda lakini leo tunashukuru limepatiwa ufumbuzi na hii itatuepusha kuingia kwenye mgogoro usio wa lazima".

# Ufuatiliaji malezi, makuzi kwa watoto wafikia 47%

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

IMEELEZWA kuwa asilimia 47 ya watoto chini ya miaka nane malezi na makuzi yao yanafuatiliwa kwa karibu, huku Mkoa wa Manyara ukiwa na asilimia 50 ya watoto wanaofuatiliwa

hayo yalielezwa na mtaalamu kutoka Mtandao wa Malezi na Makuzi ya Watoto Wadogo Tanzania (TECDEN), Bruno Ghumpi, wakati wa kikao cha mapitio ya Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi Makuzi na Maendeleo ya Awali (PJT-MMMAM),kwa kipindi cha Januari hadi Juni mwaka huu.

Ghumpi alisema hapa nchini bado wazazi, walezi na serikali hawajaweza kufuatilia ukuaji wa watoto walio chini ya miaka minane kikamilifu ili waweze kukua katika utimilifu.

**Malezi ya mtoto yanaanzia akiwa tumboni na hii ni ajenda ya kitaifa ambayo imeshikiliwa na Rais Samia Suluhu Hassan hivyo wote tuwajibike.**

Aidha, alisema mkoa ambao unafanya vizuri ni Arusha, ambao unawafuatilia watoto kwa zaidi ya asilimia 70, akisema kwa Mkoa wa Manyara katika eneo la lishe bado wana asilimia 36 za udumavu wakati kiwango cha kitaifa ni asilimia 31.

Katibu Tawala Mkoa wa Manyara, Karolina Mthapula, alisema watoto wa umri wa miaka sifuri mpaka nane ni kipindi muhimu cha kuwa nao karibu kwa malezi.

"Malezi ya mtoto yanaanzia akiwa tumboni na hii ni ajenda ya kitaifa ambayo imeshikiliwa na Rais Samia Suluhu Hassan hivyo wote tuwajibike," alisema Mthapula.

Vilevile alisema mtoto akipewa chakula vizuri kabla ya kuzaliwa na baada ya kuzaliwa humfanya kuwa bora.

Hivyo, alitumia fursa hiyo kuwaagiza maofisa elimu kuhakikisha wanajua idadi ya wanafunzi wanaokula chakula shuleni na siyo kutaja idadi ya shule zinazolisha chakula.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Cosita linalotekeleza mradi wa mtoto kwanza, Patrice Gwasma, aliwaomba wataalamu wa serikali kuendelea kusimamia utoaji wa chakula shuleni ili watoto wapate chakula na kusoma vizuri.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Mkoa wa Manyara, Anna Fisoo, alisema ili watoto waweze kukua katika utimilifu kitu cha msingi ni mama kunyonyesha vizuri.



Mwenyekiti wa Taasisi ya Jamiyatul Akhlaaqul Islam (JAI) Tanga, Suleiman Kasimu (wa pili kulia), akizungumza na wanachama wa taasisi hiyo, juzi katika hospitali teule wilayani Muheza baada ya kufanya usafi na kutoa msaada kwa wagonjwa ikiwamo sabuni, dawa za meno, vinywaji, biskuti kwa watoto pamoja na kufanya usafi. (Wa tatu kulia mwenye fagio) ni mlezi wa taasisi hiyo, Makame Seif. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Kairuki achukizwa na migogoro kazini, atoa maagizo

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, (TAMISEMI), Angellah Kairuki amewaagiza watumishi wa halmashauri nchini, kuepuka migogoro sehemu za kazi na kujikita kusimamia miradi ya maendeleo.

Aidha, ameziagiza halmashauri zote nchini pamoja na ofisi za wakuu wa mikoa, ambao hawajapanga mpango kazi katika kutekeleza miradi ya maendeleo kwa mwaka huu wa fedha, kuweka mipango hiyo.

Pia, amewaagiza wakuu wa wilaya zote nchini, kujishusha na kusikiliza kero za wananchi na kuzitatua ikiwamo kutenga siku maalum za kuwasikiliza wananchi.

Aliyasema hayo jana wilayani Karatu, wakati akifungua mafunzo kazi ya siku nne kwa viongozi wa Mkoa wa Arusha, wakurugenzi pamoja na wakuu wa idara na vitengo, kutoka halmashauri saba za Mkoa wa Arusha.

"Nyie watumishi ninawaomba muwe na mshikamano, penye dosari tujirekebishe, ili tuimarishe uhusiano katika maeneo yetu ya kazi, hasa katika kusimamia miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika maeneo yenu.

"Ndugu zangu staha, heshima, nidhamu na utawala bora ni misingi imara katika maeneo ya kazi, lakini pia chuki na fitina ziwe mwiko kwenu, lakini mjikite katika kusaidiana mtumishi mwenzenu anapopatwa na matatizo binafsi lakini isiwe kuchunguza maisha ya mwenzako," alisema.

Alisema mafunzo hayo yataongeza chachu na ufanisi hasa katika mwaka huu wa fedha ambapo serikali imetenga fedha nyingi kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

Kuhusu wakuu wa wilaya, Kairuki alisema anatambua kazi nzuri wanayoifanya, akisema lakini inahitajika nguvu zaidi katika kusikiliza kero za wananchi na kuzitatua.

Aidha, alisisitiza taarifa za ripoti hasa za lishe ziwe za uhalisia kwa kuwa baadhi ya watumishi wamekuwa wakitengeneza taarifa zisizo na uhalisia na wakati mwingine kuziwasilisha kwenye mamlaka za juu, kitu ambacho ni kinyume na utaratibu wa utumishi wa umma.

Pia, aliagiza wanafunzi wa kidato cha tano wanaoripoti shuleni kupokelewa na kuwekewa mazingira rafiki, kwa sababu wengi ni wageni, akisema endapo ikitokea upungufu mipango mbadala iwekwe ili kuondoa changamoto.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, alisema Rais Samia Hassan Suluhu ana ndoto kubwa ya kuhakikisha kila mikoa, wilaya na halmashauri zinatekeleza shughuli mbalimbali za kimaendeleo kwa wananchi.

Alisema siku nne watakazozitumia watawawezesha kukaa pamoja kwa ajili ya kufahamiana ikiwemo uboreshaji wa shughuli mbalimbali za serikali.

Mkuu wa Wilaya ya Karatu, Dadi Kolimba, alimshukuru Rais Samia kwa kufungua uchumi wa Karatu ambao umewezesha mapato ya utalii kufikia Sh. bilioni 27, huku hoteli zikiwa 68 zenye hadhi ya nyota tatu.





# Atupwa jela miaka 30 kwa kumbaka mtoto wa kufikia

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKAZI wa Mtaa wa Nyasubi Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, Mseven Mchele amehukumiwa Kwenda jela miaka 30 baada ya kukutwa na hatia ya kumbaka mtoto wake wa kufikia wa miaka 12.

Hukumu hiyo imetolewa na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Kahama, Edmund Kante ambapo mbali na hukumu hiyo pia atapigwa viboko 10 na faini ya Sh. milioni moja.

**Mahakama imemtia hatiani kwa mujibu wa Sheria Namba 130 ya Sheria ya Kanuni ya Adhabu Kifungu cha 1, 2(e)...**

Hakimu Kente alitoa hukumu hiyo baada ya kuridhika na ushahidi uliotolewa na upande wa Jamhuri ambao pasipo kuwa na shaka kuwa Mseven alitenda kosa hilo.

Alisema Mahakama imemtia hatiani kwa mujibu wa Sheria Namba 130 ya Sheria ya Kanuni ya Adhabu Kifungu cha 1, 2(e) ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 iliyofanyiwa marejeo ya Mwaka 2022.

Alifafanua kuwa Mahakama imetoa adhabu hiyo ili iwe fundisho kwake na kwa watu wengine wenye tabia kama hizo kwenye jamii ambao watatekeleza matukio ya ukatili kwa Watoto.

Awali akisoma shauri hilo wakili wa upande wa Jamuhuri, Jukael Jairo aliiomba Mahakama hiyo kutoa adhabu kali kwa Mseveni ili iwe fundisho kwake na kwa wazazi wengine wanaotekeleza matukio ya ukatili kwa watoto wao.

Nae Mseven katika utetezi wake aliiomba Mahakama hiyo impunguzie adhabu kwa madai kuwa anafamilia ya watoto watano wanaomtegemea, hoja ambayo ilitupiliwa mbali na Mahakama.




Mwenyekiti wa Kamati ya Elimu Kituo cha Taarifa na Maarifa cha Kata ya Majohe jijini Dar es Salaam, ambacho kiko chini ya Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Halima Masoud, akitoa taarifa ya shughuli mbalimbali za kamati hiyo kwenye kikao cha kituo hicho jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Makalla aipa kongole TIB kuchochea uchumi

**Na Mwandishi wetu,** MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla ameipongeza Benki ya Maendeleo TIB kwa kuchochea uchumi kupitia mitaji ya kibiashara na kuwekeza kwenye sekta mbalimbali hususani za utalii, madini, biashara, usafiri, kilimo na uvuvi.

Alitoa pongezi hizo juzi wakati wa mkutano wadau na wateja wa benki hiyo waliotoka kwenye mikoa nane ya Kanda ya Ziwa na kueleza kuwa miradi ya zaidi ya Sh. bilioni 285 imewekezwa.

Aidha, aliipongeza benki hiyo kwa kusikiliza kero za wateja wao na kupata mrejesho, akisema itasaidia benki hiyo kuboresha sera zao ili ziendane na wakati.

Alisema Mkoa wa Mwanza unakua kwa kasi kiuchumi kwani pamoja na uwepo wa fursa za kutalii, miradi mbalimbali ya miundombinu inajengwa kama Bandari, meli, Daraja la Kigongo-Busisi na Reli ya Kisasa ya SGR.

Kuhusu sekta ya uvuvi na kilimo, Makalla alisema Mkoa wa Mwanza umezungukwa na Ziwa Victoria na ardhi yenye rutuba hivyo wawekezaji wana nafasi ya kuanzisha mashamba ya kisasa hata kufufua viwanda vilivyosimama ili kuchochea maendeleo.



Naye, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo TIB, Lilian Mbassy alitoa shukrani kwa wateja, wadau wa maendeleo na watumishi wa taasisi hiyo ambao wamekua sambamba kushirikiana katika kuwainua wafanyabiashara na wadau mbalimbali.

Aliongeza kuwa malengo ya mkutano huo yalikuwa kupata maoni ya wadau ili kuwezesha benki kuboresha utoaji wa huduma kwa wateja wake.

Alisema kuwa hadi kufikia Julai 31, mwaka huu TIB imewekeza zaidi ya Sh.bilioni 285 kwenye miradi mbalimbali ndani ya sekta za kimkakati.

Alizitaja ni pamoja na maji, afya, kilimo, madini, hoteli, mawasiliano na uchukuzi, kwamba asilimia 99 ya uwekezaji huo ni miradi ya sekta binafsi.

Aidha, alisema kuwa benki hiyo ina mpango mkakati wa miaka mitano wa maendeleo na kwamba wanatoa mikopo ya mitaji ya kuanzia miaka mitatu.

## Wajawazito 1,196 waongezewa damu Hospitali ya Simiyu

**Na Ndalike Sonda,** BARIADI

WAJAWAZITO 1,190 wameongezewa damu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Simiyu katika kipindi cha Aprili hadi June mwaka huu.

Takwimu hizo zilitolewa na Mwenyekiti wa Damu Salama Mkoa wa Simiyu, Dk. Khamis Kulemba wakati akizungumza na Nipashe akieleza kuwa katika kipindi hicho uniti 3,809 za damu zilikusanywa katika kampeni mbalimbali za kuchangia damu kwa ajili ya mahitaji yaliyopo.

Alisema kuwa uniti 2,483 zilitumika kuwaongezea watu mbalimbali wenye uhitaji na kati ya hizo wajawazito liliongoza kwa kuwa na uhitaji wa uniti 1,196 likifuatiwa na kundi la watoto chini ya umri wa miaka mitano ambapo kwa kipindi hicho jumla ya uniti 531 waliongezewa.

Makundi mengine yaliongezewa damu katika kipindi hicho ni wagonjwa wa upasuaji ambapo uniti 317 zilitumika, uniti 544 wagonjwa wengine wa kawaida na uniti 132 wenye Virusi Vya Ukimwi.

Dk.Kulemba alisema kuwa kwa sasa Mkoa wa Simiyu unauhitaji mkubwa wa damu salama kutokana na kuwa na idadi kubwa ya wahitaji, huku makundi ya wajawazito na wanaojifungua, watoto chini ya umri wa miaka mitano na majeruhi ndio wenye uhitaji zaidi.

Alisema kuwa Mkoa wa Simiyu umejiwekea malengo ya kukusanya damu kwa mwaka uniti 21,116.

## Bilioni 6/- kujenga hospitali ya wilaya

**Na Vitus Audax,** MWANZA

ZAIDI ya Sh.bilioni sita zinatarajiwa kuwekezwa katika ujenzi wa ghorofa katika Hospitali ya Wilaya ya Nyamagana mkoani Mwanza itakayotoa huduma za kibingwa.

Akitoa taarifa ya ujenzi wa jengo hilo jana litakalokuwa na ghorofa nne, Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Mohamed Kiwanuka alisema ujenzi huo upo katika hatua za awali baada ya kupokea mchoro wa ramani.

Alisema jengo hilo litasaidia kuondoa msongamano wa wagonjwa katika hospitali hiyo ikiwa ni pamoja na kutoa huduma za kibingwa.

Kadhalika, alieleza kuwa katika hospitali hiyo tayari limejengwa jengo la kuhifadhia maiti lenye zaidi ya Sh.milioni 109 ambalo ujenzi wake umekamilika kwa asilimia 100.

Alisema jengo hilo kwa sasa linasubiri kuwekewa majokofu ili lianze kutoa huduma, huku hospitali hiyo ikitoa huduma kwa wagonjwa zaidi ya 172 kwa siku.

Akizungumza wakati wa ziara ya kukagua miradi ya afya, Mstahiki Meya wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza, Sima Constantine aliwapongeza viongozi wa afya kwa kuendelea kusimamia vyama vya ujenzi wa miundombinu hospitalini hapo na kuifanya kuwa na adhi ya Hospitali ya Wilaya.

Nipashe
# TESA
Jumanne Agosti 15, 2023
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI





Ukurasa 12

AZAKI zinapoingia darasani kufunzwa kufuatilia usawa wa kijinsia kwenye bajeti


Ukurasa 13

Ujio serikali mtandao majalada, barua na miadi vitakavyopungua

TEKNOLOJIA
NA PILLY KIGOME

## Itumie simu kulinda usalama nyumbani, vitega uchumi usibakie kuongea na 'Whatsap'



Kifaa cha mifumo ya ulinzi kinachofungwa katika geti kuruhusu kuingia kwa alama za utambuzi wa vidole. **PICHA: PILLY KIGOME**

MBALI na mawasiliano kama kuongea, kupata taarifa za mitandao ya kijamii na kupokea ujumbe mfupi (SMS), simu ya mkononi inatumika kwa mambo mengine mengi, ukiwamo kufungua milango na mageti nyumbani na ofisini.

Ni teknolojia inayoibuliwa na mwanafunzi Abeli Kalasoni wa Chuo cha Teknolojia na Uongozi cha Kilimanjaro (KITM), jijini Dar es Salaam.

Anasema ni mfumo unaotumia 'laini' ya simu iliyofungwa mlangoni au getini na unafungua kwa kupiga simu na geti au mlango huo unafunguka.

Huwezi kuingia ndani mpaka mwenye simu na namba ya getini aipigie, anaeleza Abeli anapozungumza na Nipashe kuhusu masuala ya uvumbuzi na ugunduzi.

Kadhalika walioko ndani ya nyumba au chumbani hawawezi kutoka mpaka kupiga simu kuwasiliana na kitasa hicho.

Anaeleza kuwa namba zinazotumiwa ni zile zinazotolewa na kampuni za simu na ni chaguo la mteja kuchagua mtandao anaoutaka.

Wakati mwingine aliyeko ndani hana lazima ya kupiga siku ili kutoka badala ya kupiga, simu mmiliki anaweza kubonyeza kitufe kinachofungua getini au mlangoni na mgeni akaondoka.

Abel anaeleza kuwa hata hivyo ili kuongeza ulinzi mlango huo hujifunga kwa muda mfupi usiozidi dakika tano.

Ubunifu zaidi chuo hapo ni ule wa wanachuo wenzake Majidi Matikiti na Japheth Fedrick, wanafunzi wa mwaka wa pili wa stashahada ya teknolojia chuoni KITM.

Wawili hao wamekuja na teknolojia nyingine ya kuingia na kutoka getini kwa kutumia mfumo wa alama za vidole (fingerprints).

Wanasema ili kuingia, mlango unafungwa kifaa kinachoweza kutambua alama za vidole ili kuruhusiwa kupita getini hapo wale alama zao zinazotambuliwa.

Akielezea ubunifu wao, mtaalamu wa mifumo ya ulinzi ya kidijitali chuoni hapo, Emmanuel Muti, anaiambia Nipashe kuwa, kinachotumika katika teknolojia hiyo ni mbinu ya kuweka kwanza alama za vidole ili mlango ufunguke.

Aidha, anasema mfumo wa kidijitali ujulikanao kama 'access control', una kifaa kinachomtambua ambaye hajasajiliwa ili kuzuia asiingie au kutoka getini hapo.

Anasema mifumo hiyo inaimarisha ulinzi zaidi kwenye nyumba, taasisi na katika majengo mbalimbali na kudhibiti uhalifu.

Muti anasema mfumo huo unaweza ukatumika kokote ukiachana na geti pia unaweza ukafunga popote ambako mtu atahitaji akitoa mfano kama gari, samani mfano kabati, jokofu na hata mashamba pia mifumo hiyo inaweza ikatumika kwa ajili ya usalama zaidi.

Anaongeza kuwa hata kama kuna wizi au uharibifu wowote unaotokea shambani unaweza kuuona kupitia mfumo huo.

"Hivyo ni rahisi kwa teknolojia hiyo kurahisisha mikakati ya usalama na ulinzi wa nyumba,ofisi, vyombo vya moto na samani kudhibiti watumiaji ambao hawajasajiliwa."

Anasema itakuwa vigumu kuingia au kutumia chochote kinacholindwa na teknolojia hiyo akiongeza kuwa kama ni familia inalazimu wote kusajiliwa kwa alama za vidole.

Mbali na geti na vitu vingine mtaalamu huyo anafafanua zaidi kuwa teknolojia hiyo inaweza ikatumika mashambani kwa kufunga mfumo huo wa usalama unaoonyesha kila kinachofanyika hata kama yuko nje ya eneo hilo.

"Inasaidia kwa kuweka usalama zaidi wa shamba, mali, mifugo na kugundua upotevu kama vile mazao, kuporwa ardhi na wafanyakazi wa shamba au majirani mipakani.

"Tumekuwa tukishuhudia watu wanaibiana ardhi ama mazao hivyo kupitia teknolojia hii ya utambuzi wa alama za vidole ni suluhisho la kuepukana na kadhia kama hizo," anasema.

Teknolojia hii ya kufungua geti kwa simù inagharimu Shilingi milion 1.8 lakini kuna ni lazima kuwa na simu na vocha lakini pia mfumo umegawanyika katika maeneo mawili wa 'manyo' na 'one line' na unapowekwa getini unaambatana na 'electronic locks' na kufuli ya umeme'

Kwa upande wa shamba linalofungwa huduma hii sio lazima liwe na uzio bali mfumo huu unafungwa juu ya nguzo kuchukua picha za shamba zim, mfumo huo unajumuisha aina mbili za teknolijia ambazo ni 'access control' , kufuli la umeme na CCTV kamera.

Mfumo huu ukifungwa shambani unakuchukua matukio yote hata kama mwenye mali atakuwa mbali na eneo hilo na unatakuwa unatumia 'access Internet' kwa kutumia simu au kompyuta, gharama inakuja pale unapohitaji kuangalia matukio ni lazima utumie bando la kutosha kujua yaliyofanyika au yanayofanyika kwa wakati unaotaka.

Gharamà ya kufunga mfumo huu ni Shilingi milioni 1.7 hii ni moja kwa moja haitagharimu tena kufanya au kuongeza fedha nyingine lakini gharama itaongezeka kwenye kifurushi au bando.

Mbezi Ahmed ni Mkuu wa Chuo cha Teknolojia na Uongozi, anayeongeza kuwa mbali na wanachuo hao waliogundua mifumo hiyo ya kiulinzi KITM, imeendelea kusomesha wataalamu mbalimbali wanaofanyakazi katika taasisi za umma na binafsi.

Anataja baadhi ya fani zinazotolewa chuoni hapo ni kompyuta, matengenezo ya vifaa, mashine na mitambo, michoro, picha, mtandao na elimu ya ukarimu na huduma za hoteli.

Mbezi anasema chuo kimekuwa na sifa na kinaendelea kutambulika zaidi kutokana na ubunifu na teknojia mbalimbali ikiwamo ya mifumo ya ulinzi kama ya kutumia alama za vidole.

Mkurugenzi Mtendaji wa KITM, Ezekiel Mpanzu, anasema taasisi hiyo inaunga mkono juhudi za serikali za kumkomboa Mtanzania kielimu hasa eneo la ufundi stadi na uhandisi.

Anasema wanaongeza ujuzi kwa kuleta watalamu mbalimbali wa ndani na nje ili kuongeza ubora wa elimu, tija na kupanua uelewa kwa wanafunzi wanaojiunga na taasisi hiyo.

ELIMU

NA SABATO KASIKA

# AZAKI zinapoingia darasani kufunzwa kufuatilia usawa kijinsia kwenye bajeti



Baadhi ya viongozi wa asasi za kiraia wakiwa katika mafunzo ya kufuatilia bajeti. **PICHA: SABATO KASIKA**

KUANZIA Agosti hadi Septemba, ni kipindi ambacho halmashauri zinawasilisha mwongozo wa mchakato wa kukusanya maoni na vipaumbele vya miradi kwa serikali za mitaa, vijiji na kata.

Ni kutokana na kwamba huu ni mwanzo wa utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2023/24 ambao ulianza Julai mosi, kazi inayoambatana na tathmini na ufuatiliaji.

Hivyo, halmashauri pia zinafanya vikao vya robo ya pili ya mwaka ambavyo vinapitisha maoni ya wananchi kuhusu miradi na vipaumbele, huku kila kijiji kikifanya mikutano hiyo muhimu.

Wakati hayo na mengi yakiandaliwa ni fursa kwa wadau kufanya utafiti na uchambuzi uchambuzi wa bajeti hiyo kama ina mrengo wa kijinsia na kufuatilia utekelezaji wake.

Ili kufanikisha hilo, Mtandao wa Jinsia Tanzania TGNP, umewaingiza darasani viongozi wa asasi za kiraia (AZAKI) kwa muda wa siku tano kwa lengo la kuwapa mbinu za ufuatiliaji huo.

Viongozi hao kutoka mikoa mbalimbali, walipata mafunzo yaliyopewa jina la ufuatiliaji wa uwajibikaji jamii katika kutoa huduma za jamii.

Katika ufunguzi wa mafunzo hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP, Lilian Liundi, anasema ushirikishwaji wa jamii katika usimamizi wa huduma unafanikisha kuchochea maendeleo na kuongeza uwezo na ari ya jamii kuona umuhimu na faida ya kodi wanayotoa.

Jamii inapopewa kipaumbele kufanya maamuzi yenye faida kwao, inakuwa ni rahisi kuleta maendeleo endelevu, na sisi TGNP tunaamini mafunzo haya yatakuwa ni nyenzo muhimu katika kufuatilia bajeti za halmashauri," anasema Lilian.

Anafafanua kuwa, ni nyenzo muhimu, kwa maelezo kwamba yatakayoiwezesha jamii kuwa na ufahamu wa jinsi gani ya kuchambua nyaraka mbalimbali za serikali za mipango na bajeti.

"Kwa miaka 30 TGNP imekuwa mstari wa mbele katika kujenga uwezo na ushawishi juu ya bajeti yenye mrengo wa kijinsia, hivyo ni imani yangu kwamba mafunzo hayo pia yatasaidia kujenga uelewa wa pamoja kwa mashirika yanayotetea haki za wanawake," anasema.

Mkurugenzi mtendaji huyo anasema uelewa wa pamoja unahusu pia mitandao ya wanawake, wanaowezesha wanaharakati ngazi ya jamii juu ya dhana muhimu zinazotumika kwenye ufuatiliaji na uwajibikaji wa jamii kwa mtazamo wa kijinsia.

"Tunataka kutengeneza mwongozo na mbinu bora za ufuatiliaji na uwajibikaji jamii kwa mtazamo wa kijinsia, kubadilishana uzoefu kwa ajili ya kuimarisha usawa wa kijinsia," anasema.

**JUKUMU**

Baada ya mafunzo hayo, sasa wanakubaliana kila mmoja kwenda kutoa elimu kwa wananchi, hasa wanawake ili watambue changamoto za eneo lao na kuziibua katika vikao.

Mwezeshaji wa mafunzo hayo Nemence Mabung'ai, anasema viongozi hao wanapata mafunzo, pia wanatakiwa kwenda kuhamasisha wananchi kuhudhuria vikao vya mitaa na kuibua changamoto za kijinsia.

"Vilevile mnatakiwa kuwajengea uwezo viongozi wa maeneo hayo juu ya umuhimu wa masuala ya jinsia kwenye changamoto zinazoibuliwa na kuziandika kwa ufasaha ili ziwasilishwe kwenye kata," anasema Mabung'ai.

Anasema elimu hiyo inatakiwa kutolewa pia katika baraza la maendeleo la kata ili kupenyeza masuala ya kijinsia kwa lengo la kuyafikisha katika ngazi ya halmashauri.

"Lakini pia halmashauri nazo zinatakiwa kujengewa uwezo, hasa kamati mbalimbali za madiwani kuhusu kujumuisha masuala ya kijinsia katika vipaumbele vilivyoibuliwa na kata," anasema.

> "Vilevile mnatakiwa kuwajengea uwezo viongozi wa maeneo hayo juu ya umuhimu wa masuala ya jinsia kwenye changamoto zinazoibuliwa na kuziandika kwa ufasaha ili ziwasilishwe kwenye kata," anasema Mabung'ai.

Aidha, mwezeshaji huyo anasema ipo haja ya kuomba ushiriki wa asasi za kiraia katika mikutano na vikao vya baraza la madiwani ili kuangalia kama kuna vipaumbele kwenye bajeti za halmashauri zao na vipaumbele vyake.

Kuna vipaumbele kwenye bajeti za halmashauri, ambavyo vimezingatia masuala ya kijinsia.

**URASIMU**

Katika mafunzo hayo, linaibuka suala la urasimu kwamba baadhi ya viongozi wa halmashauri hawako tayari kuweka wazi bajeti za halmashauri zao na vipaumbele vyake.

Hilo linaibuliwa na Bahati Simba ambaye ni Mkurugenzi wa asasi iitwayo Yowed Foundation ya jijini Dar es Salaam.

Anasema bajeti za halmashauri zimekuwa ni za siri, hali ambayo inawawia vigumu wananchi kujua vipaumbele vilivyomo.

"Nilishawahi kufuatilia bajeti katika halmashauri moja hapa Dar es Salaam, badala ya kupewa, nikaambiwa kuwa nimetumwa na vyama vya upinzani. Jibu hilo lilionyesha kuwa wananchi hawtakiwi kujua, bali wanatumwa na upinzani tu," anasema Bahati.

Anasema ingekuwa ni vyema kuondoa mtazamo huo, kwa kuwa bajeti inayohusu umma, ni muhimu waijue kuliko kuwa siri ya viongozi wakati imetengwa kwa ajili ya maendeleo ya wananchi.

Anasema mtindo huo wa baadhi ya wakurugenzi wa halmashauri unaweza kuwa kikwazo cha maendeleo, kwa maelezo kwamba si rahisi wananchi kujua kama kile wanachohitaji katika eneo lao kinazingatiwa katika bajeti hiyo.

Anaongeza kuwa pamoja na urasimu huo, kupitia

mafunzo hayo, atabadili mbinu za ufuatiliaji wa bajeti ili aipate huku akishirikisha wananchi kujua umuhimu wa ufuatiliaji kwenye maeneo hayo kuanzia katika vijiji hadi halmashauri.

Sakata la urasimu huo wa halmashauri linasemwa pia na mchambuzi wa masuala ya bajeti, Dominic Ndunguru kutoka asasi ya Open Mind Tanzania, kwamba bajeti za wizara huwa ziko wazi lakini za halmashauri haziko wazi.

"Ninadhani umefika wakati sasa halmashauri kuachana na urasimu huo ambayo kwa namba moja au nyingine unachangia wananchi kuwa gizani kwa kutojua kinachoendelea katika halmashauri zao," anasema Ndunguru.

Hata hivyo, mwezeshaji anawatia moyo kwamba kupitia mafunzo hayo, iwapo watayazingatia, itakuwa ni rahisi kufuatilia kwa njia sahihi bajeti za halmashauri zao.

"Kumekuwa na changamoto nyingi katika ufuatiliaji na uwajibikaji ikiwamo ukosefu wa rasilimali fedha na vitendea kazi, waathirika wakubwa ni wanawake, hivyo msikate tamaa, fuatilieni bajeti kwa kuzingatia maelekezo mliopewa na kupenyeza masuala ya kijinsia ili yapewe uzito," anasema.

Anasema wakati mwingine baadhi ya wafuatiaji wa bajeti wanaweza kusababisha wakose ushirikiano na kunyimwa taarifa.

"Kinachotakiwa ni kwenda na kujieleza vizuri na kuonyesha vitambulisho ili kumuondoa shaka mkurugenzi wa halmashauri au wilaya na kumfanya awe tayari kutoa ushirikiano.

"Ni kweli kwamba kama maelezo au utambulisho wako haujitoshelezi, inaweza kuwa vigumu kupata ushirikiano, lakini kwa kuwa mmeshapata mafunzo, ni imani yangu yatawasaidia kupata taarifa na kuzifanyia kazi kwenye maeneo yenu ili kuleta matokeo chanya," anasema.

Anasema Kwa kawaida serikali hupanga bajeti kulinga na vipaumbele vyake na kwamba katika mazingira hayo, wakati haizingatii mrengo wa kijinsia na kuwaacha wanawake nyuma.

Mabung'ai anasema kupitia viongozi hao waliopata mafunzo, inaweza kuwa rahisi watasaidia kuhamasisha kuwapo kwa bajeti ambayo inazingatia mrengo wa kijinsia ili kundi hilo ambalo ni kubwa linufaike na bajeti na serikali kuu hadi kwenye halmashauri.

TEKNOLOJIA
NA MWANDISHI WETU



Benedict Ndomba.

# Ujio serikali mtandao majalada, barua na miadi vitakavyopungua

## • Ni huduma kielektroniki kifanisi huku gharama zikipunguzwa

PENGINE ni Watanzania wachache wanaposikia serikali mtandao (electronic government), wanaweza kuelewa ni jambo gani hasa, au kufikiria ni nini kitakachotokea.

Kwa wepesi dhana hii inahusisha kuachana na kujaza makaratasi kwa kalamu, kuwa na vyumba vya mafaili yenye vumbi au yaliyoliwa na mchwa, kuonana na maofisa wa serikali uso kwa uso na kugonga milango ya ofisi hizo ili kupata huduma, badala yake mambo hufanywa kielektroniki.

Serikali mtandao inahusisha matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHEMA),kuwapa huduma za umma wananchi na wengine wanaoshirikiana na serikali kufanikisha majukumu mbalimbali.

Hivyo, huduma za serikali zinakuwa mtandaoni na zinawafikia watu kielektroniki iwe kuwahudumia wananchi, wafanyabiashara,wateja mahakamani, vyuoni, kwenye taasisi na vyombo vyote vya umma na hata vya kimataifa na kikanda.

Kufanikisha jitihada za serikali mtandao katika taasisi za umma kunategemea kuwapo kwa sera, sheria, kanuni, viwango, miongozo na mikakati madhubuti ili kuhakikisha matumizi sahihi na salama ya TEHAMA, katika taasisi zake yanazingatiwa, anasema, Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Serikali Mtandao (e-GA), Benedict Ndomba.

Anaiambia Nipashe kuwa usalama wa matumizi ya TEHAMA katika taasisi za umma, husaidia kulinda maslahi ya wananchi ambao ndiyo watumiaji wa huduma zitolewazo na serikali kielektroniki.

Anaongeza kuwa Sheria ya Serikali Mtandao Na 10 ya 2019, inataka kila taasisi ya umma kutekeleza miradi ya TEHAMA kwa kuzingatia viwango vya ufundi na miongozo inayoainishwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), ili kuepuka urudufu wa jitihada za Serikali Mtandao.

Ndomba anaeleza kuwa, ili teknolojia itumike serikalini lazima kuwe na usimamizi unaotoa mwelekeo wa kuhakikisha TEHAMA inayotumika, inaratibiwa na kuainisha matumizi sahihi na salama katika taasisi za umma.

Anasisitiza kwa, taasisi zote za umma kuzingatia kanuni, viwango na miongozo ya serikali mtandao katika utendaji kazi ili kujenga mifumo yenye tija na kwamba sheria inazitaka na kuzielekeza taasisi hizo kuwasiliana na e-GA ili kushirikiana na kuhakikisha matumizi ya TEHAMA yanakuwa yenye tija kwao na serikali pia.

"Mamlaka ya Serikali Mtandao ipo kwa ajili ya kuhakikisha matumizi ya TEHAMA serikalini yanakuwa yenye tija na faida kwa serikali na wananchi siyo kwa ajili ya kuzibana taasisi za umma au kuzuia matumizi ya TEHAMA," alisema.

Anasema kwa kuzingatia matakwa ya sheria hiyo, taasisi yoyote ya umma inayokusudia kutekeleza mradi wa TEHAMA inatakiwa kuwasilisha andiko la mradi e-GA, kupitia tovuti ya huduma za TEHAMA serikalini ijulikanayo kama 'Government ICT Service Portal' (GISP).

Anasema andiko hilo linapaswa kuwasilishwa wakati wa hatua ya mipango ili kupata ushauri wa kitaalam na kibali kutoka mamlakani, akifafanua kuwa kwa miradi ya TEHAMA inayoendelea au iliyokamilika, taasisi za umma zinapaswa kuwasilisha taarifa zake sahihi na kamili kupitia GISP ili e-GA ipitie na kufanya tathmini ya miradi hiyo na kutoa ushauri wa kitaalamu ikiwa kuna maeneo ya kuboresha.

"Mamlaka hufanya ukaguzi wa miradi, mifumo na miundombinu ya TEHAMA kwa lengo la kuhakikisha usalama, ufanisi pamoja na uzingatiwaji wa viwango na miongozo ya serikali mtandao, kuleta tija katika kutoa huduma bora kwa wananchi.

"Ili kufikia usalama wa mifumo, sheria ya serikali mtandao inaelekeza taasisi za umma kuhifadhi mifumo yao katika mazingira yaliyothibitishwa na serikali. e-GA inalo jukumu la kukagua mazingira yanayohifadhi mifumo hiyo kujiridhisha iwapo mazingira hayo yamethibitishwa serikalini," anasema.

Anaeleza kuwa, lengo ni kuhakikisha usalama na kwamba e-GA inaendelea kufuatilia kubaini taasisi zinazokiuka matakwa ya sheria katika kuhifadhi mifumo yao, anasema Ndomba.

"Sheria inasisitiza pale inapowezekana ujenzi wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA ifanywe kwa kutumia wataalamu wa ndani, ili washiriki kikamilifu katika ujenzi na usimamizi wa miradi na mifumo ."

Vilevile anasema washiriki kuwezesha kutatua changamoto zinazojitokeza kwa haraka zaidi akieleza kuwa sheria haijazuia kutumia wataalamu wa nje au sekta binafsi katika ujenzi wa miradi ya TEHAMA isipokuwa ni lazima miradi hiyo ifuate sheria na taratibu zilizowekwa sambamba na kukidhi viwango vya serikali mtandao.

"Katika kuhakikisha matumizi salama e-GA imeandaa viwango na miongozo mbalimbali ya serikali mtandao ambayo inatoa maelekezo na taratibu zinazotakiwa kufuatwa na taasisi za umma katika matumizi mbalimbali ya TEHAMA," anasema.

Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Serikali Mtandao anasema miongozo hiyo, inaelekeza namna ya uundaji, ununuzi, usimamiaji na utekelezaji wa jitihada za TEHAMA, jinsi ya kulinda mifumo dhidi ya maafa, majanga au uharibifu na namna ya kudhibiti athari zinazoweza kupunguza utendaji wa taasisi za umma.

Halikadhalika, anasema inaelekeza umuhimu wa matumizi bora, salama na sahihi ya mifumo, data na vifaa vya TEHAMA serikalini yatakayowezesha mifumo kuungana na kubadilishana taarifa ili kufikia dira ya kuwa na mifumo ya serikali mtandao yenye tija na ufanisi.

"Taasisi zote za umma, zinapaswa kutumia kwa ukamilifu miongozo hii ili, kuleta mafanikio chanya katika utendaji na utoaji huduma pamoja na kuhakikisha kuwa, siri za serikali hazivuji kwa kutumia mwanya wa TEHAMA na hatimaye kufikia azma ya kuwa na Serikali ya Kidijiti, ambayo inapatikana muda wowote, mahali popote na kwa hali yeyote ya mtumiaji," anaeleza.

Meneja wa Huduma za Sheria e-GA, Raphael Rutaihwa, anasema uwapo wa sheria ya serikali mtandao na kanuni zake, unasaidia kuwezesha matumizi sahihi ya TEHAMA katika taasisi za umma, yanayopelekea kuboresha utendaji kazi na kutoa huduma bora zinazopatikana kwa urahisi na haraka, na hivyo kuwa na serikali ya kidigitali iliyo imara na endelevu.

Rutaihwa anasema, sheria hiyo inazitaka na kuzielekeza taasisi za umma zinazohusika na ujenzi wa miundombinu ya serikali kama vile barabara, reli na majengo kuhakikisha kuwa, zinawekewa mazingira wezeshi kwa ajili ya kupitisha miundombinu ya TEHAMA kuanzia wakati wa kuandaa michoro ya ujenzi.

"Ili kuhakikisha tunajenga serikali ya kidijitali, ni vema taasisi zote za umma zikazingatia Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya mwaka 2019, kanuni zake pamoja na viwango na miongozo ya Serikali Mtandao iliyopo," anasema mtaalamu huyo.

SAYANSI
NA MWANDISHI WETU

# Maajabu mchakato wa kuzaliana unavyowaua viumbe hawa



Wanyama hawa hufa kewnye uzazi. Huitwa wanyama kwa vile viumbe hai huundwa na makundi mawili mimea na wanyama.
**PICHA: MTANDAO**

KUPATA mwenza unayemtaka si jambo jepesi kwa kuwa hata kwa wanyama wengi hupoteza uhai pale tu wanapokutana na wale wawapendao na wa muhimu kwao.

Ni mambo ya kustaajabisha, kwa mujibu wa BBC, kuhusu wanyama hao na kwamba wameangalia kwa ukaribu zaidi mpango wa uzalishaji unaofahamika kama 'Semelparity' au kwa maelezo mengine uzazi wa kujitoa uhai.

Mara nyingi wanyama wengi huwekeza nguvu zao nyingi kwenye kuzaliana kabla ya kufa na mmoja kati ya wanyama wa kipekee ni panya mdogo aina ya 'antechinus' wanaopatikana huko nchini Australia.

Mnyama huyu mwenye sifa za kujamiaana kwa muda wa saa 14, hali hii inapomtokea kinga ya mwili inaanza kudhoofu na hata kusababisha kifo chake muda mfupi.

Pengine unaweza kuita kujitoa mhanga kwa mzazi, panya hawa aina ya 'Antechinus' hufa katika mazingira hayo huku wakiamini kuwa wameacha mbegu na kuzisambaza watoto wengi watakaosambaa na kufika mbali zaidi.

"Jambo kubwa hapa ni kwamba spishi hizi zinapokutana huzaa watoto wengi zaidi," Jeyaraney Kathirithamby, mtaalamu wa entomolojia au elimu ya kuangalia mwanzo na mabadiliko ya viumbe hai katika Chuo Kikuu cha Oxford, anaiambia BBC.

> "Buibui wa kiume aina ya 'argiope' hupendelea kukutana na wale walio tayari kuyeyuka na mwisho hushindwa kuwala. Lakini inapotokea ni buibui mzee , atamla baada tu ya kufa ," Anasema Scott.



### KUJITOLEA KUFA

Buibui wa kike, anaelezwa kuwa anapata hisia mbaya pale tu wadudu wengine hatari wa kike wanapoamua kuwala au kuwaua wenzi wao.

Hata hivyo, buibui aina ya 'Stegodyphus lineatus' anaamua kufa kwa ajili ya watoto wake wasidhurike au kukosa chakula.

Baada ya kundi lake la kwanza la mayai kuanguliwa, mama anawatafutia chakula buibui wadogo na kisha kuwaacha wamle hadi kufa.

Anasema Catherine Scott, mwanafunzi wa uzamivu katika Chuo Kikuu cha Toronto nchini Canada.

Anaongeza kuwa buibui wa kiume ana tabia ya kujitolea miili yao ili tu waonekane kuwa ndiyo baba halisi wa buibui hao wadogo.

Buibui wa kiume "wana viungo viwili vya kuhamisha manii au mbegu za kiume, ambavyo hufahamika kama pedipalps," ambayo hutumiwa wanapokutana na buibui jike' anasema Scott.

Baada ya kufa, "mwili wa buibui wa kiume una hisia katika sehemu nyeti za buibui wa kike na hii huwapa shida buibui wengine pale wanapopata matamanio ya kukutana au kumpanda buibui huyo mjane."

"Buibui wa kiume aina ya 'argiope' hupendelea kukutana na wale walio tayari kuyeyuka na mwisho hushindwa kuwala. Lakini inapotokea ni buibui mzee , atamla baada tu ya kufa ," Anasema Scott.

### SAMAKI KIMAAJABU

Samaki huyu ni maarufu kwa kutotoa mayai mengi kupindukia. anapatikana kwenye Bahari ya Pasifiki na hufa baada ya kuzaa au kutotoa mayai.

Ni spishi wa 'chinook' ambaye husifika kwa kutotolesha mayai mpaka 5,000 kwa wakati mmoja.

Samaki jamii ya mkunga kutoka Amerika na wenyewe wanabainika kuwa hutoa mayai mpaka milioni 30 kwa wakati na muda mmoja, lakini maisha yao ya kuzaliana bado ni ya kimaajabu, anasema John Casselman, Mhadhiri wa Chuo Kikuu Ontario huko Canada.

Anasema aina hii ya samaki huchukua miaka 20 kukua, mara nyingi maisha yao wanakwenda mpaka ukingoni chini kabisa mwa bahari na hii inawapa maswali wataalamu kwani wameshindwa kufahamu wanavyozaliana, hata hivyo bado wanafanya uchunguzi wa kina zaidi kuona kama wataweza kupata njia zao.

Samaki huyu yuko hatarini zaidi kutoweka kwa sababu nyingi zinazochangiwa na uvuvi wa kupindukia na ukarabati wa mabwawa makubwa, ndiyo maana ni vigumu kufahamu siri zao za kuzaliana.

### VIFO VYA NYUKI

Wadudu nyuki jamii ya Strepsiptera, wanawake wao huzalisha kati ya mabuu 1,000 hadi 750,000 katika tendo lao moja walikutana dume na jike.

Wanyama hawa wana maisha ya kustaajabisha sana, kwa mfano wanawake huzika miili yao ndani ya mwili wa nyuki aliyekufa, akijificha lakini huzingatia kutokuwa na mabawa,macho, miguu au 'antenna', huko pia huhifadhi vitoto vyake ambavyo huonekana kama 'peremende nyeupe.'

Sehemu pekee ya mwili wao ambayo hutoka kwenye mfereji wa mwili wa mdudu aliyekufa ndiyo hupitishia watoto hapo kuna njia iliyowazi inayomwezesha mwanaume kumpanda jike na mabuu pia huitumia kutoka nje. Ni uhusiano: wataalamu wanaouita upendo wenye mahangaiko,

Vimelea vya kiume vinavyowakamata wa kike shingoni nyuki wa kiume wanaoishi kwa saa nane, ambao huruka akiwa na nyuki jike na kujamiana mpaka kifo kinapowatenganisha.

Kathirithamby anasema baada ya mabuu kutoka ndani ya mwili wa mwanamke naye pia hufa.





# NEEC yatoa Sh.trilioni 6.1 kuwawezesha wajasiriamali

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAJASIRIAMALI milioni 8.6 wamenufaika na mikopo yenye thamani ya Sh.trilioni 6.1 kupitia mifuko inayoratibiwa na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) kwa mwaka 2022/23.

Aidha, hadi kufikia Juni 2023 ajira 145,245 zimezalishwa kwa Watanzania kwenye miradi ya kimkakati na uwekezaji.

Akizungumza jana jijini hapa na waandishi wa habari, Katibu Mtendaji wa baraza hilo, Beng'i Issa kuhusu mafanikio ya masuala ya uwezeshaji Tanzania na vipaumbele kwa mwaka 2023/24.

"Hadi Machi, 2023, hii imeweza kutoa mikopo yenye thamani ya Sh. trilioni 6.1 kwa wajasiriamali 8,650,257 wakiwamo wanawake 4,747,321 na wanaume 3,902,936," alisema.

Aidha, alisema mifuko na programu hizo zimetengeneza ajira 17,603,271 ambapo ajira kwa wanawake zilikuwa 9,248,916 na ajira kwa wanaume ni 8,354,355.

**Hadi kufikia Juni 2023, jumla ya ajira 145,245 zimezalishwa kwa Watanzania kupitia miradi hii ambapo wanawake 29,049 wamenufaika na wanaume 116,196 wamenufaika.**

Kuhusu ajira za Watanzania kwenye miradi ya kimkakati, Katibu huyo alisema baraza linaratibu masuala ya ajira hiyo katika sekta za kipaumbele kama uzinduaji (mafuta na gesi), kilimo, ujenzi, viwanda, utalii na sekta mtambuka.

"Hadi kufikia Juni 2023, jumla ya ajira 145,245 zimezalishwa kwa Watanzania kupitia miradi hii ambapo wanawake 29,049 wamenufaika na wanaume 116,196 wamenufaika," alisema.

Alisema kampuni za kitanzania zaidi ya 1,700 zimenufaika kwa kupata kazi mbalimbali katika miradi hiyo.

Akizungumzia kuhusu Mpango wa Kuendeleza Viwanda Vidogo na vya Kati (SANVN Viwanda Scheme) unaolenga kutoa fursa kwa Watanzania kupata mikopo yenye riba nafuu kwa ajili ya kuanzisha na kuendeleza viwanda hususani vilivyochakata mazao ya kilimo na mifugo, alisema hadi Juni 2023 umewezesha mikopo ya Sh. bilioni 3.83 kwa miradi 65.

Alisema miradi hiyo ilifanyika katika mikoa 13 ambayo ni Mwanza, Arusha, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mbeya, Geita, Dodoma, Shinyanga, Iringa, Njombe, Singida, Pwani na Rukwa.

Kadhalika, alisema hadi Machi, 2023 vituo vya uwezeshaji 18 vimeanzishwa katika mikoa ya Shinyanga, Geita, Singida, Rukwa, Kigoma na Dodoma.

Alisema vituo viwili katika mikoa ya Morogoro na Pwani viko kwenye hatua za kuongeza huduma wezeshi na kuweza kuwa vituo vya uwezeshaji kamili.

Alisema: "Vituo hivi vimeweza kutoa mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 9.4 kwa wajasiriamali 4,017. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2022/23, serikali ilitenga fedha za kuweza kukarabati vituo katika halmashauri tatu, kwamba Nyang'wale ilipewa Sh. milioni 247, Mlele Sh. milioni 698 na Mbinga Sh. milioni 123.4".



Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Beng'i Issa, akizungumza na waandishi wa habari ukumbi wa Idara ya Habari Maelezo jijini Dodoma jana, kuhusu mafanikio ya uwezeshaji nchini na vipaumbele kwa mwaka wa fedha 2023/2024. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Usomaji mita shirikishi wapunguza malalamiko

**Na Ibrahim Joseph,** Dodoma

MKURUGENZI wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mkoa wa Dodoma (DUWASA), Mhandisi Aron Joseph, amesema usomaji wa mita za maji shirikishi umesaidia kupunguza malalamiko ya wateja wao.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini hapo alipokuwa akiwasilisha taarifa ya utendaji kazi wa mamlaka hiyo kwa ujumbe wa Bodi ya Taifa ya Maji walipotembelea ofisi za mamlaka hiyo.

Alisema usomaji huo wa mita za maji shirikishi umesaidia kupunguza malalamiko ya wateja hao kutokana na kupata taarifa ya matumizi ya kabla ya kutumiwa ankara yake ya maji aliyotumia katika mwezi husika.

Alisema ushirikishwaji huo umesaidia kubaini upotevu wa maji kutokana na kujua matumizi halisi ya wateja wao kwenye maeneo yote wanapotoa huduma hiyo ya maji.

Pia alisema wameweka namba za simu za bure za kuwasiliana na wateja wao kama kuna malalamiko na ikitokea kuna mashaka wamekuwa wakifika kwa haraka kujiridhisha na taarifa za wateja.

Kadhalika, alisema wameanza kuchimba visima kwenye baadhi ya maeneo wanayotoa huduma hiyo na lengo ni kuhakikisha kila eneo linapata maji yaliyo safi na salama.

Mwenyeti wa Bodi ya Maji ya Taifa, Mhandisi Mbogo Mfutakamba, alisema maendeleo ya uchumi dunia yanategemea upatikanaji maji ya uhakika ya matumizi.

Alibainisha kuwa maji yamekuwa ni muhimu na hayana mbadala hivyo wananchi wakiyakosa wamekuwa wakiyatafuta mbali kwa gharama kubwa.

Alisema maji hayo yaliyopo chini ya ardhi hayajatangazwa kama maeneo tengefu na ndiyo maana ukitaka kuchimba utakuta tayari maeneo yanamilikiwa na watu.

Mhandisi Mbogo alieleza kuwa serikali imeipa nguvu bodi hiyo kuhakikisha maji yanaendelea kupatikana kama nyenzo muhimu ya maendeleo ya Taifa katika kuchangia uchumi.

## Wahandisi waagizwa kusimamia miradi kikamilifu

**Na Thobias Mwanakatwe,** MKALAMA

MWENYEKITI wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), Mary Chatanda, amewaagiza wahandisi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama mkoani Singida kusimamia kikamilifu miradi inayotekelezwa wilayani humo ili ijengwe kwa ubora na viwango vinavyotakiwa.

Alitoa kauli hiyo jana wilayani hapo, baada ya kukagua miradi ya mwendelezo wa ziara yake mkoani Singida.

Alisema kuna baadhi ya miradi imekuwa inajengwa chini ya kiwango na ubora kutokana na usimamizi mbovu hivyo ni wajibu wa wahandisi kuhakikisha wanasimamia miradi hiyo ipasavyo.

Alieleza serikali inatoa fedha nyingi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali, hivyo ni vizuri miradi hiyo ijengwe kwa viwango na ubora unaotakiwa ili kudumu kwa muda mrefu.

Akikagua ujenzi wa jengo la magonjwa ya dharura la hospitali ya wilaya hiyo, aliagiza jengo hilo likamilike haraka ili wananchi waanze kupata huduma za afya.

Kuhusu tatizo la maji lililopo hospitali ya wilaya hiyo, alimpigia simu Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi na kutaka kueleza wananchi mpango wa wizara hiyo kutatua tatizo hilo.

Mahundi aliahidi kuchimba kisima cha maji hospitalini hapo ili kuondokana na tatizo hilo.

## M/kiti UWT akoshwa mradi uzalishaji ng'ombe

**Na Mwandishi Wetu,** SINGIDA

MWENYEKITI wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) Taifa, Mary Chatanda, amefurahishwa na mradi wa uzalishaji wa ng'ombe wa kikundi cha wanawake cha Tunza kilichopo Mkalama mkoani Singida.

Wanawake wa kikundi hicho ni miongoni mwa wanufaika na mikopo iliyokuwa ikitolewa na halmashauri ya wilaya hiyo, ambapo kilipata Sh. milioni 20.

Akizungumza na wanawake wa kikundi hicho, Chatanda aliwaomba wanawake hao kuendelea na uzalishaji wa ng'ombe kwa kuwa umewawezesha kurejesha fedha katika halmashauri kwa wakati.

"Niwaombe wanawake nchini kuchangamkia fursa hiyo ambayo Rais Samia Suluhu Hassan anataka mnufaike na fedha hizo. Tumuunge mkono kwa kutujali na kututhamini sisi wanawake kwa kutoa fedha bila riba" alisema.

Mary alisema UWT ipo bega kwa bega na Rais Samia katika kutatua changamoto zote za wanawake kwa kuwa ni jukumu lao, kumsaidia katika kuhakikisha wanawake nchini wanapata mikopo na wanainuka kibiashara. Alisema serikali imewashika mkono wanawake nchini kwa kuwapa fedha na kujiinua katika biashara zao, hivyo aliwaomba wasimwangushe Rais Samia kwa kuwa amewamini.

Kwa upande wa wanawake walionufaika na mradi huo wa ng'ombe akiwemo Mwenyekiti wa Kikundi cha Tunza, Jenifa Julias alimpongeza mwenyekiti huyo kwa kuwatembelea na kuwapa elimu kuhusu mikopo ya benki.





# Watu 200 wenye tatizo la mtoto jicho kutibiwa bure

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATU zaidi ya 200 waliobainika kuwa na tatizo la mtoto wa jicho mkoani Mbeya wanatarajia kupatiwa matibabu bila malipo kutokana na wengi wao kuwa ni wenye kipato cha chini.

Watu hao watapatiwa matibabu hayo katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya baada ya hospitali hiyo kwa kushirikiana na Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Maryprisca Mahundi kuandaa mpango maalumu wa kuwasaidia.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Mhandisi Mahundi ambaye pia ni Naibu Waziri wa Maji, alisema programu ya kuwasaidia wananchi hao itazinduliwa Agosti 22 mwaka huu na itafanywa na madaktari bingwa wa macho.

**Huduma hizo zitatolewa bure kwa wananchi wote wa Mkoa wa Mbeya na hivyo akawataka wananchi kujitokeza kupata huduma hiyo.**

Alisema madaktari hao watatoka Ujerumani na wengine kutoka katika Hospitali ya CCBRT ya mkoani Dar es salaam ambao watapiga kambi ya wiki moja katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya kwa ajili ya kuwatibu wananchi hao.

Aliwataka wananchi wote wenye matatizo ya macho kujitokeza katika hospitali hiyo ya kanda kwa ajili ya kufanyiwa matibabu hayo bure na kwamba watahakikisha watu wote watakaojitokeza wanatibiwa.

Alisema utaratibu huo ni mwendelezo wa nia yake ya kuwasaidia wananchi wa mkoa huo kutatua matatizo mbalimbali ambapo alisema tangu alipochaguliwa ameshatumia zaidi ya Sh. milioni 200 kuwasaidia wananchi.

Alisema moja kati ya huduma alizowasaidia wananchi ni pamoja na upasuaji kwa wanawake zaidi ya 60 waliobainika kuwa wana tatizo la fistula.

Mratibu wa huduma za macho wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya, Dk. Fariji Killewa alisema asilimia 50 ya watu wanaosumbuliwa na macho katika Mkoa wa Mbeya wana tatizo la mtoto wa jicho.

Alisema katika kipindi cha mwaka mmoja wananchi waliojitokeza katika hospitali hiyo wakiugua macho walikuwa 2,399 lakini waliobainika kuwa na tatizo la mtoto wa jicho walikuwa 1,499.

Alisema watu hao walipatiwa matibabu ya tatizo hilo kwa kufanyiwa upasuaji na kwamba tatizo hilo ni kubwa katika maeneo mengi lakini uelewa wa wananchi ni mdogo.

Alisema madaktari bingwa wa macho kutoka Ujerumani na Hospitali ya CCBRT, wataanza kazi Agosti 22 mpaka 29 mwaka huu na kwamba watashirikiana na wataalamu waliopo kuwatibu watu watakaojitokeza.

Ofisa Habari wa hospitali hiyo, Agrey Mwaijande alisema huduma hizo zitatolewa bure kwa wananchi wote wa Mkoa wa Mbeya na hivyo akawataka wananchi kujitokeza kupata huduma hiyo.

Alisema waliamua kuanzisha kampeni hiyo ya kuhamasisha wananchi baada ya kubaini kuwa baadhi ya watu wamekuwa wakishindwa kujitokeza kwenye vituo vya kutolea huduma za afya kwa sababu ya kuogopa gharama.

Alisema wengi wamekuwa wakijifungia majumbani bila kutibiwa hali ambayo inaweza ikawasababishia upofu ambao ni tatizo kubwa zaidi.



Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, akizungumza na waandishi wa habari juzi kuhusu mpango wake wa kushirikiana na Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya kuwafanyia upasuaji wa mtoto wa jicho wananchi wenye tatizo hilo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## NIC rasmi yatambulika kimataifa utoaji huduma bora

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Bima Tanzania (NIC) limepokea cheti cha ubora kutoka kwa Taasisi ya Superbrands ya kuwa kinara katika sekta hiyo ikiwa ni baada ya kufanyika kwa utafiti na tathmini ya kina ya huduma zake.

Kutambuliwa kwa NIC kunaonesha namna kampuni hiyo ilivyojikita katika kuboresha viwango vya juu vya ubora, kuwajali wateja na kuzingatia weledi.

Mkurugenzi Mtendaji wa NIC, Dk. Elirehema Doriye, alisema cheti hiko ni heshima taasisi hiyo.

"Ni heshima kubwa kupokea cheti cha utambulisho kutoka kwa taasisi ya Superbrand. Kutambuliwa huku ni uthibitisho wa kazi kubwa tunayoifanya pamoja na kujitolea kwa kila mfanyakazi wa NIC, inatuongezea chachu zaidi ya kuendelea kuboresha viwango vya huduma katika bima," alisema.

Aliongeza kuwa shirika hilo limejizatiti kuendelea kuleta maendeleo chanya kwa jamii na kuchangia kwenye shughuli za kijamii na kiuchumi kwa maendeleo ya taifa.

"Kutambuliwa na Superbrand kumekuja wakati sahihi na kuongeza ari zaidi ya NIC kuendeleza ubora wa viwango vya hali ya juu, kutumia ubunifu na teknolojia ili kuwapatia wateja huduma wanazohitaji na kusaidia sekta nzima kusonga mbele zaidi," alisema.

Alisema NIC kwa muda mrefu linajiendesha kama kinara katika soko la huduma za hisa nchini, likihudumia mahitaji ya wateja kwa kuwapatia huduma tofauti za bima ambazo zinalinda maisha, mali, na biashara zao.

# Wakazi Chunya waiangukia serikali kupata majisafi

**Na Ashton Balaigwa,** CHUNYA

WANANCHI wa Mji wa Chunya mkoani Mbeya, wameiomba serikali kuwasaidia kutatua kero ya upatikanaji wa maji ya bomba inayoukabili mji huo.

Wamesema kero hiyo inawasababishia gharama za maisha kuwa juu na kuwa katika hatari ya kukumbwa na magonjwa ya mlipuko.

Walitoa kilio hicho juzi kwenye mkutano wa hadhara ulioitishwa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera uliokuwa na lengo la kusikiliza kero za wananchi ambapo walisema kutokana na tatizo hilo wanalazimika kununua maji kwa bei kubwa.

Mmoja wa wananchi hao, Safia Hamad alisema tatizo hilo linakuwa kubwa zaidi kipindi cha kiangazi ambapo maji huwa hayatoki kwenye mabomba.

Alisema serikali iliwapelekea mradi wa kuchimba visima virefu vya maji ambavyo hutumika kuvuta maji na kujaza kwenye matangi lakini kipindi cha kiangazi visima hivyo huwa vinakauka na hivyo kuwasababisha kukosa kabisa huduma hiyo.

Zena Shabani ambaye ni mkazi wa Kitongoji cha Ujenzi alisema kipindi cha kiangazi wananunua maji kwa vijana ambao wanazungusha kwa kutumia maguta huku wakiwa hawana uhakika na usalama wa maji hayo.

Alisema wananunua ndoo moja ya lita 20 kwa Sh. 1,000 jambo ambalo alisema linawasababishia gharama za maisha kuwa juu kuliko uwezo wao wa kiuchumi.

Alisema wapo baadhi ya matajiri ambao wamechimba visima na wanawauzia lakini maji hayo yana magadi mengi.

Diwani wa Kata ya Itewe, Alex Kinyama alikiri uwepo wa tatizo hilo na kwamba mradi wa visima haukufanya vizuri kutokana na miamba ya eneo hilo kuwa na mipasuko inayosababisha maji kupotea kwa kuzama chini.

Alisema Wilaya ya Chunya ni miongoni mwa wilaya zitakazonufaika na mradi wa kupeleka maji kwenye miji 28 nchini na kwamba mradi huo ndio utakuwa suluhisho la tatizo la upatikanaji wa huduma hiyo.

Alisema wamepatiwa zaidi ya Sh. bilioni 11 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo huku akieleza kuwa wameanza kupata wasiwasi kutokana na mkandarasi aliyepata tenda ya kutekeleza mradi kutaka kubadili chanzo.

Alisema Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi pamoja na wataalamu wa Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) waliridhia chanzo cha maji cha Mto Gwaziva ambao upo umbali wa kilomita 30 kutoka kwenye mji huo ndicho kitumike.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Homera aliagiza Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Wilaya ya Chunya (CHUWASA), kuhakikisha wanatafuta suluhisho la muda mfupi wakati taratibu za utekelezaji wa mradi wa miji 28 zikiwa zinaendelea.

Vilevile alimtaka mkandarasi anayetekeleza mradi huo kwenda kuripoti kwenye ofisi yake ili apewe wataalamu watakaomshauri namna ya kutekeleza mradi huo vizuri.

Aliwataka viongozi wa serikali katika wilaya hiyo pamoja na madiwani kuhakikisha wanashirikiana na mkandarasi huyo atakapoanza kazi ili mradi huo ukamilike mapema.



# Bundi waongeza idadi ya watalii Msitu wa Amani

**Na Rahma Suleiman,** aliyekuwa

MUHEZA

NDEGE aina ya bundi katika Hifadhi ya Msitu wa Asili wa Amani uliopo Muheza mkoani Tanga wamekuwa kivutio kwa watalii wanaofika katika msitu huo.

Mtafiti wa ndege kutoka Shirika la Uhifadhi wa Ndege na Mazingira Tanzania, Edigar Apolinary, aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari kutoka Chama cha Mazingira Tanzania (JETI).

Wanahabari hao walitembelea msitu huo kwa ufadhili wa USAID Tuhifadhi Maliasili.

Apolinary alisema bundi anafaida nyingi hasa kwa wakulima, kwamba huondoa wadudu waharibifu wanaoshambulia mazao ikiwamo panya buku.

Mtafiti huyo anapingana na imani na fikra za baadhi ya wananchi wanaoamini kuwa ndege huyo anamambo mabaya ikiwamo uchuro, nuksi na ushirikina.

Alisema katika msitu huo ndege huyo ni kivutio kikubwa cha utalii na anaongeza fedha za kigeni na pato la taifa kutokana na watalii na watafiti wanaofika katika msitu huo.

**Mimi namuona bundi kama ndege wengine hii ni kutokana na elimu niliyopata kutoka shirika lisilo la kiserikali linalohusika na uhifadhi wa ndege na mazingira Tanzania na tunashirikiana na wanakijiji wezangu pamoja na serikali katika kuwalinda.**

Aidha, alisema ndege huyo ni tofauti na ndege wengine kwa sababu huonekana zaidi nyakati za usiku na hata watalii wanaofika katika msitu huo huwalazimu kufanya utalii nyakati za usiku ili kumuona.

Mkazi wa Kijiji cha Magoda ambacho kimezungukwa na hifadhi ya msitu huo, Habibu Chando alisema elimu zaidi inahitajika kwa jamii kuhusu umuhimu wa ndege akiwamo bundi kwa sababu wengi wao wanamuona ndege huyo katika mtazamo hasi.

"Mimi namuona bundi kama ndege wengine hii ni kutokana na elimu niliyopata kutoka shirika lisilo la kiserikali linalohusika na uhifadhi wa ndege na mazingira Tanzania na tunashirikiana na wanakijiji wezangu pamoja na serikali katika kuwalinda," alisema.

Kaimu Mhifadhi wa Hifadhi ya msitu huo, Alphonce Nyululu anasema hifadhi hiyo hupokea watalii wengi wanaofika kuangalia ndege akiwemo bundi, utalii wa vinyonga na utalii wa maporomoko ya maji.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2007/2008 hadi 2022/ 2023 hifadhi hiyo imeingiza Sh. milioni 538 baada ya kupokea watalii 14,096.

Alisema katika hifadhi hiyo wanavifaa vya kisasa ambao huvitumia waongoza watalii katika msitu huo kwa kumuita bundi.

Mkurugenzi Mtendaji wa JETI, John Chikomo, alisema waandishi wa habari wananafasi kubwa ya kuuhabarisha umma umuhimu wa misitu pamoja na viumbe hai vinavyopatikana ikiwemo ndege.

Alisema bila ya uwepo wa misitu ni hatari kubwa kwa taifa lakini pia viumbe hai waliopo wakiwemo ndege aina ya bundi watatoweka.

Alisema viumbe hai husaidia katika kulinda bayoanuai lakini pia katika kukuza pato la taifa kunakotokana na sekta ya utalii.

Mkurugenzi huyo alisema lengo la ziara hiyo kwa waandishi wa habari ni kuangalia Shoroba ya Amnai-Niro kwa sababu ni miongoni mwa shoroba muhimu kwa uhifadhi wa bayoanuai nchini.

Aidha, alisema shoroba hiyo inavivutio mbalimbali ambavyo havipatikani katika shoroba zingine ikiwemo ndege aina ya bundi.



Meneja Mradi wa Ufugaji wa Vipepeo, Amiri Sheghembe, akizungumza na waandishi wa Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JETI) waliofanya ziara katika Msitu wa Asili wa Amani Muheza mkoani Tanga, ziara iliyoandaliwa na JETI kwa ufadhili wa mradi wa USAID tuhifadhi maliasili. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Ujenzi Kituo cha Polisi Tumbatu kumaliza kero ya uhalifu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAMISHNA wa Polisi Zanzibar, Hamad Khamis Hamad, amesema kukamilika kwa mradi wa Kituo cha Polisi Kisiwa cha Tumbatu kutatatua changamoto za kiusalama katika kisiwa hicho.

Aliyasema hayo huko mkoa wa Kaskazini Unguja alipokuwa akikagua mradi wa ujenzi wa Kituo cha Polisi Tumbatu.

Alisema kituo hicho kitakapokamilika kitatoa huduma kwa wananchi kwa wakati na kwa urahisi kwa sababu kabla ya ujenzi huo wanachi wa kisiwa hicho wakifuata huduma katika Kituo cha Polisi Mkokotoni hali ambayo inawalazimu kuvuka bahari.

Naye Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kaskazini Unguja, Kamishna Msaidizi Daniel Shila, alisema kituo hicho kitawapunguzia wanachi gharama wanapohitaji huduma za kipolisi na kuwasisitiza wananchi kuendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi na kuhakikisha wanaitunza miundombinu hiyo.

Wananchi wa kisiwa hicho waliipongeza serikali kwa kuwasogezea huduma hiyo karibu, waliwaomba askari watakao pangiwa katika kituo hicho wajengewe makazi kisiwani hapo.

"Tunaiomba serikali kituo kitakapoanza kufanya kazi watendaji wake wapatiwe makazi katika kisiwa hiki na isiwe wanakuja asubuhi alafu jioni wanaondoka kwa sababu wahalifu hawana muda maalum," alisema Miza Makame mmoja wa wakazi wa kisiwa hicho.

Kituo hicho kimegharimu zaidi ya milioni 250 hadi kukamilika kwake na hadi sasa ujenzi wake umefikia asilimia 70.

**Kituo hicho kimegharimu zaidi ya milioni 250 hadi kukamilika kwake na hadi sasa ujenzi wake umefikia asilimia 70.**

# Uwanja wa Ndege Abeid Karume kufungua uwekezaji

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Zanzibar imesema Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume Pemba na Barabara ya Chakechake hadi Wete utafungua mlango wa uwekezaji katika sekta ya utalii kisiwani humo.

Hayo yamesemwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, alipokuwa akizungumza katika sherehe za uzinduzi wa mradi wa Cocco lagoon wa nyumba za makazi na bangaloo.

Alisema kwamba kuimarika kwa huduma za miundombinu kutaimarisha sekta ya utalii na huduma za usafirishaji na uchukuzi hasa baada ya wawekezaji kuanza kujitokeza kuwekeza katika Kisiwa cha Pemba.

Chini ya mpango huo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, inatarajia kutumia Sh. trilioni 1.4 kujenga kilomita 103 za miundombinu ikiwemo Uwanja wa Ndege Pemba kuwa wa kimataifa, Barabara ya Mkoani/Chake, Tunguu/ Makunduchi na Kisauni/Fumba.

Aidha, alisema wakati mipango ya ujenzi wa barabara hizo ukiendelea kampuni ya ujenzi wa Mecco inaendelea na ujenzi wa barabara ya Cheke/Wete ambayo itaunganisha mikoa miwili ya Pemba na kuimarisha huduma za usafirishaji na uchukuzi.

Soraga alisema ndani ya muda mchache Pemba itafunguka kiuchumi ambapo itasaidia katika ustawi wa jamii na kusukuma gurudumu la maendeleo katika kisiwa hicho.

Alisema kunahitajika mikakati ya mapema ya kuongeza uzalishaji wa mazao ya vyakula na mazao ya baharini kutokana na ukuaji wa sekta ya utalii unaondelea kujitokeza kisiwani Pemba ili kuepusha kutegemea bidhaa hizo nje ya visiwa hivyo.

Ofisa Miliki wa Bodi ya Kondominia inayohusika na makazi katika mradi huo, Salim Muhammed alisema mradi huo utasaidia kuongeza ajira kwa vijana na kutangaza sekta ya uwekezaji visiwani Zanzibar.

Alisema nyumba zinazoendelea kujengwa eneo la Wambaa Mkoa wa Kusini pemba, kupitia mradi huo zitasajiliwa na bodi hiyo kwa watu watakaonufaika pia ni utekelezaji wa mpango wa serikali kwa kukuza uchumi kupitia uchumi wa buluu Zanzibar.

Naye Meneja Mauzo na Uendeshaji wa Kampuni ya Cocco lagoon, Jakub Kazmierczak alisema mpaka sasa nyumba 24 zimeuzwa tangu kuanza mauzo ya awali ya nyumba za makazi katika mradi huo zikiwa na huduma zote muhimu.

Alisema uwekezaji huo umezingatia uhifadhi wa mazingira na kulinda rasilimali lakini utasaidia kukuza uchumi wa Zanzibar na kutangaza sekta ya utalii kimataifa kisiwani humo.

NUSU YA MADAKTARI KUFELI

# Serikali yaunda kamati kuchunguza

**Na Jenifer Gilla**

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, ameunda kamati yenye wajumbe 13, kuchunguza malalamiko ya madaktari tarajali wanaodai kuwapo ukiritimba katika mitihani ya kupata leseni ya taaluma hiyo inayosimamiwa na Baraza la Madaktari Tanganyika (MCT).

Ni uamuzi uliochukuliwa na serikali baada ya Julai 21, mwaka huu wawakilishi hao kumwandikia Rais Samia Suluhu Hassan barua ya wazi yenye hoja kadhaa zinazohusu malalamiko hayo na nakala yake kupelekwa Wizara ya Afya.

Katika taarifa yake kwa umma jana, Waziri Ummy alisema kamati hiyo itakayoongozwa na Mganga Mkuu wa Serikali mstaafu, Prof. Muhamad Bakari, itafanya kazi kwa mwezi mmoja kwa kufuata hadidu za rejea zilizoainishwa na wizara ili kuchunguza msingi wa malalamiko yaliyotolewa na madaktari tarajali hao.

Vilevile, Waziri Ummy alibainisha kuwa katika muda ambao kamati hiyo itakuwa inatekeleza majukumu yake, taratibu zingine za mafunzo ya madaktari tarajali zitaendelea kama ilivyoainishwa kisheria.

Aliwata madakatari tarajali kuwa na subira katika kipindi ambacho kamati inafanya uchunguzi na pale watakapohitajika kutoa maelezo kwa kamati, watoe ushirikiano kwa kuwa wizara itasimamia haki na ustawi wa taaluma ya udaktari nchini.

Daktari Bingwa wa Tiba ya Familia kutoka Hospitali ya Agakhan jijini Dar es Salaam, Willbroad Kyejo, alipongeza uamuzi wa serikali kuunda kamati hiyo ikiwa na wajumbe madaktari wabobevu watakaokwenda kuchunguza suala hilo kitaalamu zaidi.

Alisema anaamini matokeo ya uchunguzi huo yatatoa majibu yatakayoridhisha pande husika na kama kuna tatizo mahali, busara itatumika kutatua changamoto hiyo.

"Ninaamini pia wanafunzi hao watapewa nafasi ya kuzungumza kama kuna changamoto walipitia wakati wanafanya mitihani hiyo na wakipewa mitihani ya marudio watafanya vizuri zaidi. Lengo liwe kujenga, siyo kubomoa," alishauri.

Aliongeza: "Udaktari ni fani muhimu sana kwa kuwa inahusisha moja kwa moja afya na uzima wa binadamu. Kwahiyo, ni lazima wasimamizi wajiridhishe kuwa daktari ameiva inavyostahili kabla ya kupewa kibali cha kutoa huduma kwa jamii."

Daktari Daraja la Pili katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Amosi Kilipamwambu, alisema kuundwa kamati hiyo kunatoa ishara serikali inajali wananchi wake na imedhamiria kutenda haki kwa pande zote mbili.

Alisema kufanya mitihani ya aina hiyo si suala jipya. Linafanyika dunia nzima kwa lengo la kujiridhisha daktari anayehitimu anaweza kutoa huduma kwa wananchi kwa namna inayostahiki.

"Kwa mfano, leo mimi nikiomba kazi Marekani ni lazima nifanye huo mtihani na kuna bodi inasimamia, ili wajiridhishe kuwa ninaweza kuifanya kazi hiyo vizuri. Kwa sababu unaweza kuwa daktari lakini ukashindwa kufanya baadhi ya majukumu," alisema Dk. Amos.

Zaidi ya nusu ya madaktari tarajali waliofanya mtihani wa kuipata leseni hiyo mwaka huu wameanguka. Kati ya 640 walioufanya, 366 (asilimia 57) wamefeli.

Katika mazungumzo na Nipashe jijini Dar es Salaam wiki mbili zilizopita zilizopita, mwakilishi wa madaktari tarajali hao, Baraka Shija, alidai zaidi ya wahitimu 300 wa fani ya udaktari waliofanya mtihani huo mwaka huu wamefeli.

Shija alidai kufeli kwao katika mtihani huo kumetokana na alichokiita urasimu ndani ya MCT, ikiwamo kuwataka wafanye mtihani wenye maswali 200 ndani ya saa tatu.

Katika ufafanuzi wake kwa Nipashe kuhusu suala hilo, Dk. David Mzava, Msajili MCT, alibainisha kuwa madaktari tarajali 640 walifanya mtihani wao Machi 22 mwaka huu. Kati yao, 274 (asilimia 43) walifaulu na 366 (asilimia 57) walifeli, akikiri kwamba idadi ya waliofanya vibaya ni kubwa.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza na wananchi Stendi Kuu wilayani Newala, akiwa kwenye ziara ya siku mbili mkoani Mtwara jana. **PICHA: OWM**

# PM aahidi maboresho huduma za afya nchini

**Na Mwandishi Wetu, NEWALA**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali inaendelea kuboresha huduma mbalimbali za kijamii nchini zikiwamo za afya, hivyo wananchi waendelee kuipa ushirikiano.

Alitoa rai hiyo jana alipozungumza na wananchi baada ya kuweka jiwe la msingi katika Hospitali ya Wilaya ya Newala akiwa katika ziara ya kikazi mkoani Mtwara.

Waziri Mkuu alisema serikali imedhamiria kuendelea kuboresha huduma za afya nchini, huku akimwagiza Mkuu wa Wilaya ya Newala asimamie ipasavyo upatikanaji dawa katika vituo vya kutolea huduma za afya kwa kuwa serikali inatoa fedha nyingi kwa ajili ya kugharamia huduma hiyo.

Waziri Mkuu alisema serikali kila mwezi inapeleka fedha kwa ajili ya ununuzi wa dawa, hivyo hatarajii wananchi wanaokwenda vituo vya kutolea huduma za afya wakose dawa.

Mganga Mkuu wa Wilaya, Dk. Matiko George, alisema serikali imetoa Sh. bilioni 2.85 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali ikiwamo jengo la maabara, wagonjwa wa dharura, huduma ya mama na mtoto, mionzi, utawala, wodi za wanawake, wanaume na watoto.

Alisema faida za mradi huo ni pamoja na kupunguza gharama kwa wananchi ambao walilazimika kutembea umbali mrefu kufuata huduma za afya katika halmashauri za jirani za Newala Mji, Masasi na Hospitali ya Rufani Ndanda.

"Hospitali hii itakuwa na uwezo wa kufanya huduma za upasuaji kwa kinamama watakaokuwa wanapata changamoto ya kujifungua kwa njia ya kawaida. Pia huduma za afya za kinywa na macho nazo zitatolewa hospitalini hapa," alisema.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

KATIKA MAHAKAMA YA RUFANI YA TANZANIA
INAYOKETI DAR ES SALAAM

SHAURI LA MAOMBI YA GHARAMA NA. 24 OF 2023

LTA CONSTRUCTION (TANZANIA)
LIMITED……………………………MLETA MAOMBI WA 1
PETER SCHUMAN ……………………MLETA MAOMBI 2
AVENG LIMITED……………………MLETA MAOMBI WA 3

DHIDI YA

RESOLUTE (TANZANIA) LIMITED ………MJIBU MAOMBI

KWA:
RESOLUTE (TANZANIA) LIMITED

POPOTE ULIPO

Unajulishwa kwamba shauri la maombi ya gharama tajwa hapo juu limepangwa kusikilizwa na Mahakama hii hapa Dar es Salaam tarehe 11/09/2023 saa tatu kamili asubuhi (3.00).

Unapaswa kuhudhuria siku na tarehe iliyopangwa bila kukosa na endapo hutahudhuria wewe wenyewe au mwakilishi wako anayetambulika kisheria basi maombi haya yatasikilizwa bila ya uwepo wako.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa Mahakama hii leo tarehe 02/08/2023.

THE COURT OF APPEAL OF TANZANIA

J. E. FOVO
Kny: MSAJILI
MAHAKAMA YA RUFANI



KUPOTEA KWA CHETI



**PRISCA GEORGE MWAMBONA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye index **No S 0341/167** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia **SANGU SECONDARY SCHOOL** mwaka **2013**. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**Taarifa polisi: MBE/MBE/RB/690809/2020.**



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA MBINGA

MBINGA

SHAURI LA MAOMBI YA GHARAMA NO. 1/2023

(Lililotokana na Shauri la Madai Na. 12/2023 Mahakama ya Wilaya Mbinga)

KATI YA

AMSEK SECURITY SERVICE LIMITED………………MLETA MAOMBI

DHIDI YA

CHINA HENAN INTERNATIONAL CO OPERATION GROUP COMPANY LIMITED (CHICO LTD)……………………MJIBU MAOMBI

KWA: CHICO LTD.

Unaamuriwa kufika Mahakamani tarehe **16/08/2023** saa mbili na nusu asubuhi siku ambayo shauri la maombi ya gharama tajwa hapo juu limepangwa kwaajili ya kutajwa.

Imetolewa kwa amri yangu na muhuri wa mahakama hii leo tarehe **11/08/2023.**

MBINGA DISTRICT COURT TANZANIA

A.A. MKAMA
HAKIMU MKAZI MKUU
MAHAKAMA YA WILAYA MBINGA

DISTRICT RESIDENT MAGISTRATE
P.O.BOX 11
MBINGA

# Serikali ya kijeshi Niger kumshtaki rais aliyeondolewa

**NIAMEY, Niger**

SERIKALI ya kijeshi nchini Niger imesema itamfungulia mashtaka Rais aliyeondolewa madarakani Mohamed Bazoum kwa uhaini na kudhohofisha usalama wa ndani na nje ya taifa hilo.

Ilielezwa jana kuwa taarifa hiyo ilikuja saa chache baada ya kundi la wanazuoni waandamizi wa Kiislamu kusema viongozi wa mapinduzi ya nchi hiyo wako tayari kwa diplomasia kutatua mzozo wao na jumuiya ya kikanda ya Afrika Magharibi.

Bazoum, 63, na familia yake wamezuiliwa katika makazi rasmi ya rais huko Niamey tangu mapinduzi ya Julai 26, mwaka huu, huku wasiwasi wa kimataifa ukiongezeka juu ya hali zao kizuizini.

Rais aliyeondolewa madarakani alisema kwamba matibabu ambayo yeye na familia yake wamepokea ni ya kikatili, huku serikai ya kijeshi ikisema baada ya daktari kumtembelea Bazoum kwamba hakukuwa na matatizo yoyote kuhusu afya yake.

Msemaji wa Jeshi la Niger Kanali Maj Abdramane, ambaye alisoma taarifa hiyo kwenye televisheni ya taifa, pia alishutumu vikwazo haramu, na vya kufedhehesha vya Jumuiya ya Kiuchumi ya Afrika Magharibi (ECOWAS).

**BBC**



Wafanyakazi wa uokoaji wakiwapeleka wahamiaji ufukweni, baada ya boti iliyokuwa imewabeba kutoka Ufaransa kuzama katika njia ya maji Dover, Uingereza juzi. **PICHA: MTANDAO**

# Usalama duni waiondoa MINUSMA Mali

**BAMAKO, Mali**

UJUMBE wa kulinda amani wa Umoja wa Mataifa nchini Mali, (MINUSMA), umesema kuwa umeharakisha uondokaji kutoka kambi ya kaskazini mwa nchi hiyo kutokana na hali ya usalama inayozidi kudorora.

Siku chache zilizopita, muungano wa waasi unaoongozwa na wapiganaji wa kabila la Tuareg, unaoitwa Uratibu wa mavuguvugu ya Azawad, (CMA), umevituhumu vikosi vya jeshi la Mali na wapiganaji wa kundi la Russia la Wagner, kukiuka makubaliano ya kusitisha mapigano kwa kuvishambulia vikosi vyake vilivoko mjini Ber.

Ilielezwa kuwa Jeshi la Mali halijajibu tuhuma hizo, licha ya kusema wanajeshi wake sita walioko Ber waliuawa wakati wakizima jaribio la uvamizi na makundi ya magaidi wasiojulikana. Huku likieleza kuwa limechukuwa udhibiti wa kambi ya Ber baada ya matukio kadhaa yaliyovuruga usafiri wa vikosi vyake.

MINUSMA ulizisihi pande zote husika kujizuia na hatua zozote zinazoweza kuongeza ugumu katika operesheni zao, licha ya kutowataja waliohusika.

Pia inaelezwa kuwa makabiliano hayo yamesababishwa na madai ya kushtukiza ya Mali kwa MINUSMA kuhitimisha ujumbe wake wa muongo mzima, na kuibua wasiwasi kwamba kuondoka kwake huenda kukazidisha ugumu katika utekelezaji wa makubaliano ya amani ya 2015 na waasi wa Tuareg na kudhohofisha juhudi za kudhibiti uasi.

Taarifa zilisema ufafanuzi kuhusu tarehe ya mwanzo ya uondokaji havikutajwa, lakini katika ujumbe uliochapishwa jana na kikosi hicho kilisema msafara wa MINUSMA ulioondoka Ber ulishambuliwa mara mbili, na kwamba walinda amani watatu waliojeruhiwa walihamishiwa mjini Timbuktu kwa ajili ya matibabu.

Taarifa hiyo iliongeza kuwa mashambulizi dhidi ya walinda amani yanaweza kuwa uhalifu wa kivita chini ya sheria ya kimataifa.

Ujumbe wa MINISUMA, uliokuwa na wanajeshi 11,600 na maofisa wa polisi 1,500 nchini Mali, ulianza mwaka 2013 baada ya uasi wa wanaotaka kujitenga na wapiganaji wa jihadi kuzuka kaskazini mwa Mali.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa kitendo cha MINISUMA kujiondoa Mali kumezidisha mzozo kati ya utawala wa kijeshi na waasi wa zamani wa vuguvugu la CMA.

CMA ilisema kwamba jeshi la Mali lilikuwa limedhamiria kukalia maeneo ya MINUSMA kwa gharama yoyote ile, ikiwemo maeneo yalio chini ya udhibiti wa CMA, katika ukiukaji wa makubaliano ya amani ya 2015.

**DW**

## Papa ashtushwa idadi wanaofia baharini

**VATICAN, Italy**

MKUU wa Kanisa Katoliki Papa Francis amesema idadi ya wahamiaji wanaofia kwenye bahari ya Mediterranean ni jeraha la wazi kwa ubinadamu baada ya wiki nzima iliyogubikwa na mfululizo wa ajali za boti.

Katika ibada ya kila wiki ya Angelus, kiongozi huyo mwenye umri wa miaka 86 aliwaombea watu 41 walioripotiwa kupotea siku chache zilizopita na wenzao wanne walionusurika na kupelekwa kwenye kisiwa cha Italy cha Lamepdusa.

Papa alisema ni maumivu na aibu, huku akikumbusha takwimu za Umoja wa Mataifa (UN), zikionyesha kwamba zaidi ya wahamiaji 2,000 wamekufa kwenye bahari ya Mediterranean tangu mwanzoni mwa mwaka huu.

Wakati huohuo pia aliwapongeza wote wanaojihusisha na kuzuia ajali za boti pamoja na uokozi.

Msemaji wa shirika la UN linaloshughulikia wakimbizi, (IOM) mwishoni mwa wiki alisema kwamba takribani watu 2,060 wamekufa kwenye bahari ya Meditarrenean tangu mwanzoni wa mwaka, wakati 1,800 miongoni mwao wakipoteza maisha katikati ya bahari hiyo kati ya Afrika kaskazini kuelekea Italy na malta.

**VOA**

## Mazungumzo serikali na upinzani yaendelea Kenya

**NAIROBI, Kenya**

AWAMU nyingine ya mazungumzo ya kujaribu kupata muafaka kati ya serikali ya Kenya na upinzani, inatarajiwa kuendelea tena huku kukiwa na matumaini ya kupatikana makubaliano.

Inaelezwa kuwa hilo linatarajiwa kijiri baada ya wiki kadhaa za maandamano ya upinzani, kulalamikia kupanda kwa gharama ya maisha na shinikizo za kuifanyia marekebisho Tume ya Uchaguzi.

Ilibainishwa kuwa kikao hicho kinaendelea kuratibiwa na rais wa zamani wa Nigeria, Olusegun Obasanjo, na kwamba kinatarajiwa kutoa suluhu ya mvutano unaoendelea kati ya kinara wa upinzani Raila Odinga na serikali, ambako kila upande ulichagua timu ya watu watano.

Mchambuzi wa masuala ya siasa Kenya Dk. Brian Mutie, alisema "Mazungumzo yatazaa matunda iwapo pande zote mbili ziko kwenye hali ya kuweka mambo wazi".

Aidha, makundi ya kutetea haki za binadamu nchini humo yalisema karibia watu 30 walifariki katika maandamano yaliyoitishwa na Odinga, huku upinzani ukisema rekodi zake zilionyesha watu 50 waliuawa.

Upinzani ulisimamisha maandamano mwezi Aprili na Mei ili kuruhusu mchakato sawa wa mazungumzo ya pande mbili, lakini maandamano yalianza tena baada ya mazungumzo kuvunjika.

**RFI**

HABARI MICHEZO

# PLUIJM AFURAHIA NGAO YA JAMII IMEWABEBA AFRIKA

**Na Saada Akida, TANGA**

LICHA ya malengo yake kutotimia, Kocha Mkuu wa Singida Fountain Gate FC, Hans Van der Pluijm, amesema mashindano ya Ngao ya Jamii yamemsaidia kuimarisha kikosi chake kuelekea michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika ambayo watashiriki.

Singida Fountain Gate imemaliza katika nafasi ya nne baada ya kupoteza mechi ya mshindi wa tatu waliyocheza dhidi ya Azam FC.

Kikosi cha timu hiyo tayari kimerejea Dar es Salaam ili kujiandaa na mchezo wa Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya JKU ya Zanzibar utakaopigwa Agosti 18, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex na marudiano wiki moja baadaye.

Akizungumza na Nipashe jana, Pluijm alisema malengo yao yalikuwa ni kutwaa taji hilo lililochukuliwa na Simba lakini mechi mbili walizocheza zimewasaidia wachezaji wake kuimarika zaidi.

Pluijm alisema amepata mwanga wa kuona madhaifu yao ikiwamo safu ya ushambuliaji na ulinzi ambayo ilikuwa na makosa katika mechi dhidi ya Azam FC ambayo walifungwa mabao 2-0.

"Hatukufikia malengo yetu lakini hii michezo imetusaidia kuandaa kikosi kuelekea mechi yetu ya Kombe la Shirikisho, haitakuwa mechi rahisi kwa sababu wapinzani wetu wamejipanga vizuri.

Hayo mashindano sio rahisi kwa sababu timu zilizofanikiwa kucheza michuano hii walifanya vizuri katika ligi zao, hatutawadharau kwa sababu tunahitaji kusonga mbele katika michuano hiyo," Pluijm alisema.

Singida Fountain Gate yenyewe itaanza kampeni ya kuwania taji la Ligi Kuu Tanzania Bara kwa kuwakaribisha Prisons Agosti 22, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM Liti, mkoani Singida.

Pazia la Ligi Kuu Bara litafunguliwa rasmi leo kwa Ihefu kuwakaribisha Geita Gold FC wakati Dodoma Jiji itawaalika Coastal Union na JKT Tanzania itawafuata Namungo mkoani Lindi.



Baadhi ya Wafanyakazi wa Kampuni ya Barrick nchini wakishiriki mbio za riadha za CRDB Marathon zilizofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kakolanya aipania Ligi Kuu

**Na Faustine Feliciane, TANGA**

BAADA ya timu yake kutoka mikono mitupu katika mashindano ya Ngao ya Jamii, kipa wa Singida Fountain Gate, Beno Kakolanya, amesema yuko tayari kwa mikikimikiki ya Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo itaanza rasmi leo.

Kakolanya alisema timu yake imefanya maandalizi mazuri na anaamini makosa yliyojitokeza katika michuano iliyomalizika juzi jijini hapa watayafanyia kazi na hatimaye kuwa na msimu mzuri wa mwaka 2023/2024.

Kipa huyo amesema ana uhakika sasa kiwango chake kitaongezeka kutokana na kupata nafasi ya kucheza mara kwa mara baada ya kujiunga na timu hiyo mpya akitokea Simba.

"Nina imani kubwa na timu yangu kufanya vizuri, kila mmoja kwenye kikosi anataka kusaidia timu kufanya vizuri, tumemaliza michuano hii na sasa nguvu zetu zinahamia katika mashindano ya kimataifa, tunaenda kupambana," alisema Kakolanya.

Aliongeza anatarajia msimu mpya utakuwa mgumu kutokana na uimara wa timu zote ambazo zimejiimarisha kwa ajili ya kuonyesha ushindani.

"Mimi nadhani msimu ujao ligi itakuwa ngumu zaidi, timu zimesajili kwa kadiri ya nguvu zao, ligi itakuwa ngumu na ninamaanisha ushindani utaongezeka sana," Kakolanya alisema.

## Wavu washindwa kwenda Cameroon

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Taifa ya Wanawake ya wavu imeshindwa kuelekea Cameroon katika mashindano ya Afrika kutokana na ukata wa fedha, imefahamika.

Mashindano ya Afrika ya wavu yalianza jana na yatamalizika Agosti 25, mwaka huu.

Katibu wa Kamati ya Timu za Taifa wa Chama cha Wavu Tanzania (TAVA), Riziki Godwin, alisema jana ukata umechangia kushindwa kuisafirisha timu yao na hivyo wamepoteza nafasi ya kutimiza malengo yao.

"Tumefanya maandalizi ya muda mrefu lakini timu yetu imeshindwa kwenda katika mashindano, inatusikitisha sana, wachezaji wamejisikia vibaya mno, tutajipanga upya kwa ajili ya kushiriki mashindano yajayo," alisema Godwin.

Amewataka wachezaji kutokata tamaa kwa changamoto waliyokutana nayo ambayo imewavuruga na kuharibu kalenda yao ya mashindano.

## Mwenyekiti Simba kuzikwa leo Tanga

**Na Renatha Msungu DODOMA**

MWENYEKITI wa zamani wa klabu ya Simba, Ayoub Chamshama, aliyefariki India alipopelekwa kwa ajili ya matibabu anatarajiwa kuzikwa leo, imeelezwa.

Mtoto wa marehemu, Chamshama Soud, aliliambia Nipashe mazishi ya baba yake yatafanyika katika kijiji cha Kilole, Lushoto jijini, Tanga.

"Tuna masikitiko makubwa ya kutangaza kifo cha baba yetu mpendwa Ayoub Saleh Chamshama kilichotokea Agosti 11, mwaka huu huko India alipokuwa anapatiwa matibabu, kwa Dar es Salaam msiba uko Chang'ombe Maduka Mawili," alisema Soud.

"Uongozi wa Simba unatoa pole kwa ndugu, jamaa na marafiki walioguswa na msiba huu, tuko pamoja na familia katika kipindi hiki kigumu cha maombolezo ya kumpoteza mpendwa wetu," ilisema taarifa ya Simba.

Enzi za uhai wake, marehemu Chamshama alikuwa mwenyekiti wa Simba katika kipindi cha kuanzia mwishoni mwa miaka ya 1980 na baadaye mwanzoni mwa mwaka 2000.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### NEYMAR SAFARI IMEIVA
MSHAMBULIAJI wa Paris St-Germain na Brazil, Neymar mwenye umri wa miaka 31, amekubali mkataba wa misimu miwili na klabu ya Saudi Pro League ya Al-Hilal ambayo itampatia euro milioni 160 - mradi tu ada ya uhamisho itakubaliwa. **(L'Equipe)**

### CAICEDO, CHELSEA SAFI
KIUNGO wa kati wa Brighton na Ecuador, Moises Caicedo mwenye umri wa miaka 21, jana alitarajiwa kufanyiwa vipimo vya afya katika klabu ya Chelsea kabla ya kukamilisha uhamisho wa pauni milioni 115. **(TalkSport)**

### BALOGUN KUMRITHI KANE
KLABU ya Tottenham Hotspur inafikiria kumnunua mshambuliaji wa Arsenal, Folarin Balogun, mwenye umri wa miaka 22 baada ya nyota wake, Harry Kane kuondoka. **(Gazzetta Dello Sport)**

### SANGARE AGOMBEWA ULAYA
LIVERPOOL, Bayern Munich na Paris St-Germain zinavutiwa na kiungo wa kati wa PSV Eindhoven mwenye umri wa miaka 25 aliyekadiriwa kuwa na thamani ya pauni milioni 32, Ibrahim Sangare. PSV ilikataa ofa kutoka Nottingham Forest msimu huu wa joto. **(ESPN Uholanzi)**

### BAYERN YAIKATALIA UNITED
KLABU ya Bayern Munich imekataa ofa ya Manchester United ya kumnunua beki wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Benjamin Pavard mwenye umri wa miaka 27. **(Sky Sports)**

### ONANA AKARIBIA UNITED
MANCHESTER United inafikiria kumnunua kiungo wa kati wa Ubelgiji, Amadou Onana, mwenye umri wa miaka 21, na wanasubiri kujua bei yake kutoka kwa Everton. **(Mail)**

### AJAX YAMFUATA AKPOM
KLABU ya Ajax inatazamiwa kumsajili mshambuliaji wa zamani wa England, Chuba Akpom, mwenye umri wa miaka 27 kutoka Middlesbrough kwa dau la pauni milioni 10. (Subscription - Athletic)

### WALKER KUBAKIA CITY
MLINZI Kyle Walker mwenye umri wa miaka 33 anatarajia kusaini mkataba mpya na Manchester City wiki hii baada ya kukataa kuhamia Bayern Munich. **(Fabrizio Romano)**

### CITY YAMWINDA OLISE
KLABU ya Manchester City itamfikiria kiungo wa kati wa Crystal Palace na Ufaransa, Michael Olise mwenye umri wa miaka 21, ikiwa watashindwa kumsajili kiungo wa kati wa West Ham na Brazil, Lucas Paqueta (25). **(Football Insider)**

### LAVIA AKARIBIA LIVERPOOL
LIVERPOOL inatarajiwa kufikia ofa ya Chelsea ya pauni milioni 55 kwa kiungo wa kati wa Southampton na Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Romeo Lavia, mwenye umri wa miaka 19. **(TalkSport)**

### JUVE, CHELSEA WATETA
JUVENTUS ipo katika mazungumzo na Chelsea kuhusu kumsajili mshambuliaji wa Ubelgiji, Romelu Lukaku, mwenye umri wa miaka 30, ambaye ameonyesha nia ya kuhamia Turin. **(Corriere Dello Sport)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# NEYMAR AKARIBIA KUSAJILIWA SAUDIA

Ni baada ya ndoto zake za kurejea Barca kukwama huku uamuzi...

**PARIS, Ufaransa**

MSHAMBULIAJI wa Paris Saint-Germain, Neymar anakaribia kukubaliana na maslahi binafsi ya Al Hilal na kukamilisha uhamisho wa kwenda Ligi Kuu ya Saudi Arabia, kwa mujibu wa ESPN.

PSG wanataka euro milioni 80 kwa ajili ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, lakini mazungumzo kati ya klabu hizo yanaendelea vizuri, vyanzo vimesema.

Vyanzo viliongeza Neymar anatazamiwa kusaini mkataba wa miaka miwili wenye thamani ya euro milioni 100 kwa mwaka huko Al Hilal, ambapo anaweza kuungana na Kalidou Koulibaly, Rúben Neves na Sergej Milinkovic-Savic.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil aliachwa nje ya kikosi cha PSG kwenye mechi yao ya ufunguzi ya Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, Jumamosi wakati wakitoka suluhu na Lorient, huku kukiwa na ripoti za kuondoka klabuni hapo.

Kurejea Barcelona kulikuwa ni pendekezo, huku nahodha wake, Sergi Roberto akisema alijadiliana na Neymar.

ESPN iliripoti mapema wiki hii Neymar ameonyesha nia ya kujiunga tena na Barcelona msimu huu wa joto, lakini kuna mjadala wa ndani katika klabu kuhusu usajili wa mshambuliaji huyo, na wengine wakipinga - akiwamo kocha, Xavi Hernandez.

Uwezekano wa kuhamia Barca ulionekana ni mdogo kwa sababu ya matatizo ya kifedha ya klabu na upinzani wa Xavi kutomtaka.

Vyanzo viliiambia ESPN kuwa PSG, ambao walimsajili fowadi, Ousmane Dembélé, kutoka Barca Jumamosi iliyopita na wangefurahi Neymar kuondoka.

Tangu alipohamia Ufaransa mwaka wa 2017, Neymar ameshinda mataji matano ya Ligue 1 na mataji 13 ya nyumbani kwa jumla, na pia kumaliza mshindi wa pili katika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya za mwaka 2020.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,144,17

JACKPOT
MECHI WIKI HII
TAREHE: 17 NA 18 AGOSTI 2023
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 17/08/23 | 19:00 | HJK Helsinki vs Karabakh | 2.55 | 3.46 | 2.50 |
| 02. 17/08/23 | 20:00 | Levski Sofia vs Hapoel Beer Sheva | 2.36 | 3.10 | 3.00 |
| 03. 17/08/23 | 20:00 | Austria Vienna vs Legia Warszawa | 2.55 | 3.46 | 2.50 |
| 04. 17/08/23 | 20:30 | Breidablik vs Zrinjski Mostar | 2.50 | 3.46 | 2.55 |
| 05. 17/08/23 | 21:00 | Neman Grodno vs NK Celje | 2.70 | 3.25 | 2.49 |
| 06. 17/08/23 | 21:00 | NK Osijek vs Adana Demirspor | 2.60 | 3.30 | 2.55 |
| 07. 17/08/23 | 22:00 | Libertad Loja vs Delfin SC | 2.70 | 3.21 | 2.39 |
| 08. 17/08/23 | 22:00 | Debreceni VSC vs Rapid Vienna | 2.69 | 3.19 | 2.54 |
| 09. 18/08/23 | 01:00 | Londrina PR vs Atletico GO | 2.57 | 3.11 | 2.57 |
| 10. 18/08/23 | 13:00 | Avispa Fukuoka vs Niigata Albirex | 2.25 | 2.90 | 3.00 |
| 11. 18/08/23 | 13:30 | Urawa Red Diamonds vs Nagoya Grampus | 2.18 | 2.97 | 3.18 |
| 12. 18/08/23 | 13:30 | Incheon Utd vs Gwangju | 2.50 | 2.98 | 2.67 |
| 13. 18/08/23 | 13:30 | Suwon Samsung vs Jeju Utd | 2.63 | 3.03 | 2.50 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# XAVI AKERWA NA REFA BARCELONA IKISHIKWA



**BARCELONA, Hispania**

KOCHA wa Barcelona, Xavi Hernandez, amemjia juu mwamuzi wa LaLiga baada ya timu yake kuanza kutetea taji la Ligi Kuu Hispania kwa suluhu dhidi ya Getafe hapo juzi na kusema anaharibu mchezo huo.

Pande zote mbili zilimaliza mtanange mkali wa wachezaji 10 baada ya Raphinha na Jaime Mata kutolewa nje kwa kadi nyekundu, huku Xavi naye akitolewa nje kipindi cha pili.

Xavi alisema mwamuzi, Cesar Soto alikuwa ameiruhusu Getafe kupita kiasi na akamshutumu kwa "kubuni" mpira wa mkono dhidi ya Gavi ili kuepuka kuipa Barca penalti ya dakika za lala salama kwa kumchezea vibaya, Ronald Araújo.

"Hii ilikuwa ni mechi isiyopendeza," alisema Xavi akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo kwenye Uwanja wa Coliseum Alfonso Perez.

"Kama hii ni bidhaa ligi tunayoiuza ni aibu kabisa, huo ndio ujumbe usiku wa leo (juzi), kila mtu ameona hilo, inabidi ukweli usemwe tusikae kimya.

"Mwamuzi aliruhusu kila aina ya upuuzi, alinitoa nje katika nafasi ya kwanza na akasema mpira wa mkono wa Gavi. Muda uliopotezwa ulikuwa wa aibu. Tungesimamisha saa kwa sababu huu ni ujinga."

Barca walikasirishwa mapema na matukio kadhaa ambayo hayakuadhibiwa, ikiwa ni pamoja na ukaguzi wa mwili wa Damián Suárez, ambao ulizua hali ya uhasama ambayo Xavi alisema ilisababisha Raphinha kutolewa nje.

"Kadi nyekundu ya Raphinha ni mwisho wa mambo," alisema bosi huyo wa Barca.

"Jukumu liko kwa viongozi. Kwangu, lilikuwa kubwa sana. Tulipoteza vichwa vyetu na Raphinha alifanya makosa, lakini kwa sababu mambo mengi yalikuwa yametokea."

# Mbappé sasa kubaki PSG

**PARIS, Ufaransa**

KYLIAN Mbappé yuko katika mazungumzo ya kuongeza mkataba wake na Paris Saint-Germain na klabu hiyo sasa ina uhakika atasalia, kwa mujibu wa ESPN.

Mbappé alirejeshwa katika kikosi cha kwanza cha PSG Jumapili baada ya mvutano wa muda mrefu na klabu hiyo ambao ulimfanya kukosa ziara ya kujiandaa na msimu mpya barani Asia na mechi ya ufunguzi ya kampeni ya Ligue 1 dhidi ya Lorient.

Vyanzo viliiambia ESPN kufuatia mazungumzo mazuri Jumamosi, Mbappé alikubali na kuahidi kutoondoka kwa uhamisho wa bure mkataba wake utakapomalizika mwakani.

Rais wa klabu hiyo, Nasser Al-Khelaifi, aliwaambia waandishi wa habari kuhusu kukubaliana na Mbappé.

Nahodha huyo wa Ufaransa aliadhibiwa na kusimamishwa kwa kukataa kuongeza mkataba wake.

PSG pia ilimworodhesha kuuzwa na walikuwa wakisikiliza ofa za mshindi huyo wa Kombe la Dunia la mwaka 2018.

Mbappé, mfungaji bora wa Ligue 1 katika misimu mitano iliyopita, alikuwa akifanya mazoezi na wachezaji wengine wa PSG wanaouzwa, wakiwamo Georginio Wijnaldum, Julian Draxler na Leandro Paredes.

PSG watarejea kwenye mechi ya Ligue 1 dhidi ya Toulouse Jumamosi.



72,464/-

# JKT QUEENS YANG'ARA MICHUANO YA CECAFA

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara, JKT Queens imeanza vyema kampeni ya kusaka ubingwa wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA) baada ya kuifunga AS Kigali Women mabao 2-1 katika mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Omondi Lugogo, Uganda juzi jioni.

Haikuwa rahisi kwa mabingwa hao kupata ushindi huo kwani ilianza kuruhusu bao dakika ya pili lililowekwa wavuni na Zawadi Usanase na kukifanya kikosi hicho cha Maafande kuongeza juhudi.

Kabla ya mapumziko, Stumai Abdallah, aliisawazishia JKT Queens bao



hilo baada ya kuunganisha faulo iliyopigwa na Happiness Hezron.

Kipindi cha pili kila timu ilifanya mabadiliko na hatimaye Donisia Minja alikwamisha mpira wavuni na kuipatia JKT Queens goli la ushindi.

Kwa matokeo hayo yanawaweka wawakilishi hao wa Tanzania Bara katika nafasi nzuri ya kuelekea kwenye kampeni ya kutwaa ubingwa wa CECAFA ili kupata tiketi ya kushiriki fainali za Ligi ya Mabingwa Afrika kwa wanawake.

Kocha Mkuu wa JKT Queens, Esther Chabruma, alisema ushindi huo umetokana na jitihada za wachezaji wake na wataendelea kupambana kuhakikisha wanasonga mbele katika michuano hiyo.

JKT Queens itashuka tena dimbani kesho kucheza mechi ya pili dhidi ya New Generation FC ya Zanzibar ambayo juzi ilipata kichapo cha mabao 3-1 kutoka kwa Vihiga Queens ya Kenya.



Wachezaji wa timu ya mpira wa kikapu ya Dynamos wakifanya mazoezi maalum ili kujiimarisha kwenye Uwanja wa JMK Park, Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Yanga yamfungua macho Robertinho

INATOKA UK. 24

timu inapokuwa na mechi, hali hii inaongeza hamasa kwa wachezaji," alisema kocha huyo.

Naye Kocha wa makipa wa Simba, Daniel Cadena, amefichua siri ya ubora wa Ally Salim kudaka penalti unatokana na mazoezi waliyokuwa wakifanya mara kwa mara.

"Ninafuraha sana kuona Ally anafanya kile alichofundishwa kwenye uwanja wa mazoezi, kwa ubora alionyesha katika mechi hizi, matarajio yangu anazidi kuimarika kila siku," alisema Cadena.

Naye Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, alisema wachezaji wake walijituma kusaka ushindi lakini hawakuwa na bahati ya kufunga kupitia nafasi mbalimbali walizotengeneza.

Gamondi alisema timu yake ilikuwa ni bora zaidi, ninafurahishwa na kiwango kilichoonyeshwa lakini nimeumizwa na kupoteza kwa kufungwa katika hatua ya penalti," Gamondi alisema.

"Hatukufanikiwa kufunga, sisi tulikuwa bora zaidi, ninafurahishwa na kiwango kilichoonyeshwa lakini nimeumizwa na kupoteza kwa kufungwa katika hatua ya penalti," Gamondi alisema.

Aliongeza mechi ilikuwa ya ushindani mkubwa, ilikuwa bado bora kwake kucheza na Simba ni timu bora, lakini wachezaji wake walikosa umakini katika kutengeneza nafasi na walishindwa kuzitumia walizopata.

Nahodha wa Yanga, Bakari Mwamnyeto, alisema suala la penati halina mwenyewe lakini kiujumla timu yao ilicheza vizuri katika kila eneo.

"Kilichokosekana kilikuwa ni kufunga mabao tu, kuweka mpira wavuni, lakini tulicheza vizuri sana, tukutane katika ligi," Mwamnyeto aliongeza.

Tayari timu zote zimesharejea Dar es Salaam tayari kwa ajili ya mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo pazia lake litafunguliwa leo kwa michezo mitatu.


## SUPA JACKPOT
## MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 19/08/23 | 17:00 | Fulham FC vs Brentford FC | 2.55 | 3.25 | 2.60 |
| 02. 19/08/23 | 19:15 | Caykur Rizespor vs Alanyaspor | 2.36 | 3.25 | 2.55 |
| 03. 19/08/23 | 19:30 | Tottenham Hotspur vs Manchester United | 3.00 | 3.40 | 2.21 |
| 04. 19/08/23 | 19:30 | Empoli FC vs Hellas Verona | 2.35 | 3.15 | 2.95 |
| 05. 19/08/23 | 21:45 | Hatayspor Antakya vs Kasimpasa Istanbul | 2.32 | 3.35 | 2.60 |
| 06. 19/08/23 | 21:45 | Genoa CFC vs ACF Fiorentina | 2.95 | 3.25 | 2.30 |
| 07. 19/08/23 | 22:30 | Portimonense SC vs Boavista Porto | 2.43 | 3.10 | 2.90 |
| 08. 19/08/23 | 22:30 | CA Osasuna vs Athletic Bilbao | 2.75 | 3.05 | 2.60 |
| 09. 20/08/23 | 14:30 | VfL 1899 Osnabruck vs FC Nuremberg | 2.48 | 3.40 | 2.60 |
| 10. 20/08/23 | 14:30 | Holstein Kiel vs FC Magdeburg | 2.35 | 3.55 | 2.70 |
| 11. 20/08/23 | 16:00 | Le Havre AC vs Stade Brest 29 | 2.55 | 3.20 | 2.65 |
| 12. 20/08/23 | 16:00 | FC Lorient vs OGC Nice | 3.05 | 3.40 | 2.18 |
| 13. 20/08/23 | 17:30 | Estoril Praia vs Rio Ave FC | 2.40 | 3.15 | 2.90 |
| 14. 20/08/23 | 18:00 | Hamarkameratene vs Rosenborg BK | 2.70 | 3.25 | 2.26 |
| 15. 20/08/23 | 19:00 | FC Sudtirol Bolzano vs Spezia Calcio | 3.15 | 2.95 | 2.15 |
| 16. 20/08/23 | 20:15 | KV Kortrijk vs KAS Eupen | 2.15 | 3.45 | 3.10 |
| 17. 20/08/23 | 21:45 | RC Lens vs Stade Rennes | 2.33 | 3.50 | 2.75 |


## MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMANNE - 15/08/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 11:00 | 5532 | Spain W vs Sweden W | 2.12 | 3.21 | 3.16 |
| 13:00 | 1449 | Sangju Sangmu vs Seoul E Land | 1.51 | 4.23 | 4.73 |
| 13:00 | 3116 | Oliveirense vs CD Feirense | 2.42 | 3.28 | 2.66 |
| 13:30 | 1136 | Busan I Park vs Jeonnam Dragons | 1.92 | 3.43 | 3.38 |
| 18:00 | 3134 | Nasaf Qarshi vs Pakhtakor | 2.24 | 2.85 | 3.10 |
| 18:00 | 3776 | Mamelodi Sundowns vs Golden Arrows | 1.45 | 4.21 | 6.16 |
| 18:00 | 4631 | Seinajoen JK vs FC KTP | 1.47 | 3.87 | 5.84 |
| 19:30 | 3939 | Nublense vs Union La Calera | 2.37 | 3.17 | 2.76 |
| 20:00 | 1930 | Aris Limassol vs Rakow Czestochowa | 2.22 | 3.23 | 3.03 |
| 20:00 | 5419 | Maccabi Haifa vs Slovan Bratislava | 1.60 | 3.62 | 5.35 |
| 20:00 | 5916 | Sparta Prague vs Copenhagen | 2.12 | 3.26 | 3.21 |
| 20:30 | 4309 | Chippa Utd vs Orlando Pirates | 4.33 | 3.19 | 1.83 |
| 21:00 | 3900 | Dinamo Zagreb vs AEK Athens | 2.12 | 3.26 | 3.21 |
| 21:00 | 4251 | Backa Topola vs Sporting Braga | 4.45 | 3.79 | 1.66 |
| 21:00 | 4579 | Galatasaray vs Olimpija Ljubljana | 1.32 | 4.90 | 7.80 |
| 21:30 | 3128 | Sturm Graz vs PSV Eindhoven | 3.03 | 3.41 | 2.14 |
| 21:30 | 3339 | Aberdeen FC B vs Peterhead | 3.42 | 3.83 | 1.83 |
| 21:30 | 4907 | Brechin City vs Hibernian B | 2.13 | 3.76 | 2.75 |
| 21:30 | 5955 | Servette Geneva vs Rangers | 2.99 | 3.27 | 2.23 |
| 21:45 | 1073 | Annan Athletic vs Stranraer | 1.93 | 3.65 | 3.25 |
| 21:45 | 1491 | Loughgall vs Glentoran Belfast | 6.05 | 4.33 | 1.40 |
| 21:45 | 1685 | Wrexham vs Walsall | 1.57 | 3.92 | 4.81 |
| 21:45 | 1715 | Derby vs Oxford Utd | 2.19 | 3.40 | 3.05 |
| 21:45 | 1723 | Morecambe vs Notts County | 3.47 | 3.38 | 1.94 |
| 21:45 | 1873 | Carlisle vs Wigan | 2.56 | 3.36 | 2.56 |
| 21:45 | 1909 | Crawley Town vs MK Dons | 3.47 | 3.38 | 1.94 |
| 21:45 | 2028 | Forest Green vs Swindon Town | 2.43 | 3.29 | 2.60 |
| 21:45 | 2072 | Carrick Rangers vs Coleraine FC | 4.04 | 3.49 | 1.74 |
| 21:45 | 2243 | Cambridge Utd vs Stevenage | 2.32 | 3.30 | 2.90 |
| 21:45 | 2258 | Doncaster vs Mansfield | 3.49 | 3.44 | 1.91 |
| 21:45 | 2508 | Charlton vs Bristol Rovers | 2.17 | 3.56 | 2.96 |
| 21:45 | 2575 | Shrewsbury vs Burton | 2.20 | 3.35 | 3.05 |
| 21:45 | 2587 | Tranmere vs Harrogate | 2.04 | 3.14 | 3.43 |
| 21:45 | 2638 | Northampton vs Lincoln | 2.56 | 3.36 | 2.56 |
| 21:45 | 2905 | Crewe vs Newport | 2.61 | 3.15 | 2.51 |
| 21:45 | 2946 | Grimsby vs Salford City | 2.60 | 3.18 | 2.50 |
| 21:45 | 3803 | Crusaders Belfast vs Dungannon Swifts | 1.21 | 5.45 | 9.89 |
| 21:45 | 4106 | Blackpool vs Port Vale | 1.71 | 3.75 | 4.39 |
| 21:45 | 4687 | Bolton vs Fleetwood Town | 1.71 | 3.84 | 4.29 |
| 21:45 | 4708 | Wycombe vs Leyton Orient | 2.19 | 3.39 | 3.04 |
| 21:45 | 4749 | Albion Rovers vs Tranent Juniors | 2.43 | 3.62 | 2.43 |
| 21:45 | 4783 | Barnsley vs Peterborough | 2.19 | 3.39 | 3.04 |
| 21:45 | 5814 | Newry City AFC vs Cliftonville Belfast | 4.54 | 3.88 | 1.58 |
| 21:45 | 5885 | Linfield Belfast vs Glenavon | 1.27 | 4.96 | 8.09 |
| 21:45 | 5912 | Larne vs Ballymena Utd | 1.17 | 6.49 | 10.14 |
| 22:00 | 1875 | Reading vs Cheltenham | 2.19 | 3.40 | 3.05 |
| 22:00 | 2517 | Marseille vs Panathinaikos | 1.54 | 3.91 | 5.35 |
| 22:00 | 4488 | Portsmouth vs Exeter | 2.07 | 3.46 | 3.26 |
| 22:00 | 4763 | O Higgins vs Magallanes | 2.11 | 3.14 | 3.25 |
| 23:00 | 3733 | Colon Santa Fe vs Lanus | 3.36 | 2.90 | 2.19 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumanne Agosti 15, 2023
Nipashe



Neymar akaribia kusajiliwa Saudia UKURASA 21

# YANGA YAMFUNGUA MACHO ROBERTINHO

●●●Mbrazili huyo asema haikuwa kazi rahisi kubeba Ngao huku Mwamnyeto akilia...

**Na Saada Akida, TANGA**

WAKATI Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliviera 'Robertinho', akisema ubingwa wa Ngao ya Jamii umemwonyesha mwanga mzuri kuelekea msimu mpya, watani zao Yanga wamesema hawakuwa na bahati ya kufunga katika mechi hiyo ya fainali na sasa wanaelekeza nguvu kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Simba iliwavua ubingwa Yanga baada ya kupata ushindi wa penalti 3-1 katika fainali iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM, Mkwakwani jijini Tanga juzi usiku.

Akizungumza na Nipashe jana, Robertinho alisema furaha yake ya kuchukua taji la kwanza tangu aanze kukinoa kikosi cha timu hiyo alipokuja msimu uliopita imeongezeka zaidi kwa sababu amepata taji hilo kupitia mechi ya dabi.

Robertinho alisema ameshinda mataji mbalimbali katika timu alizozifundisha awali ila ndani ya kikosi cha Simba anajua pia amewafurahisha mashabiki na wanachama wa timu hiyo.

"Haikuwa mechi rahisi kushinda, niwapongeze wachezaji wangu kujituma hadi mwisho na kufanikisha kile tulichokitarajia, nina furaha kupata taji langu la kwanza hapa, ni jambo kubwa ambalo linatupa dira kuelekea msimu mpya wa mashindano.

Nimechukua mataji matatu nikiwa Rwanda na matatu nikiwa Uganda, lakini kwa hapa Tanzania hili la kwanza, ninawapongeza wachezaji, benchi la ufundi na viongozi kwa kufanikisha hili," alisema Robertinho.

Kocha huyo alisema licha ya kundi moja la wachezaji kuwafiti lakini wameonyesha uwezo mzuri na kila mmoja kufanya majukumu yake hatimaye walifikia malengo ya kutwaa taji hilo.

Aliongeza safu ya ulinzi ya timu yake imeimarika na ilifanya vizuri katika kuzuia mashambulizi kutoka kwa wapinzani wao ambao walikuwa wakifika katika eneo lao la hatari.

"Nawapongeza mashabiki wetu, wanaipenda sana timu yao, mara zote wanajitokeza kwa wingi uwanjani kila

INAENDELEA UK. 23



Kipa wa Yanga, Djigui Diarra (kushoto), akiruka kuwania mpira dhidi ya kiungo wa Simba, Clatous Chama katika mechi ya fainali ya Ngao ya Jamii iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini, Tanga juzi usiku. Simba ilishinda kwa penalti 3-1. **PICHA: SIMBA SC**

## Tambo zatawala Ligi Kuu Bara ikirindima leo

**Na Adam Fungamwango**

TIMU sita zinatarajia kushuka katika viwanja vitatu tofauti nchini kuanza kampeni ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambao unashikiliwa na Yanga ya Dar es Salaam.

Mechi ya ufunguzi wa ligi hiyo msimu huu itachezwa kwenye Uwanja wa Highland Estates ulioko Mbarali, Mbeya kwa wenyeji Ihefu kuwakaribisha Geita Gold kutoka mkoani Geita kuanzia saa 10:00 jioni.

Ni kama marudio ya msimu uliopita kwa timu hiyo ilipowaalika Ruvu Shooting, mchezo ulimalizika kwa Ihefu kuchapwa bao 1-0, mfungaji akiwa ni Ally Bilal dakika ya 18.

Wenyeji watashuka na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 3-1 walioupata kwenye uwanja huo hapo Juni 6, mwaka huu lakini ikipoteza ugenini kwa bao 1-0.

Mechi nyingine itakayochezwa leo ni kati ya Namungo FC watakaokuwa nyumbani Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa, Lindi, saa 12:00 jioni kuwaalika JKT Tanzania iliyorejea Ligi Kuu msimu huu baada kuteremka msimu wa 2020/21.

Meneja wa Namungo, Idris Bandari, amesema baada ya mazoezi yao ya muda mrefu katika kambi yao iliyokuwa Karatu, Arusha na baadaye Dar es Salaam, kikosi chao kiko tayari kuanza Ligi Kuu Bara.

"Tulicheza mechi kadhaa za majaribio, sasa ni zamu ya kuwapa furaha mashabiki wetu kwa kuchukua pointi tatu kwenye uwanja wa nyumbani," alisema meneja huyo.

Kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma, Dodoma Jiji itawavaa Coastal Union, mchezo utakaochezwa kuanzia saa 3:00 usiku.

Msemaji wa Dodoma Jiji, Moses Mpunga, alisema kampeni yao ya kuhakikisha wanashinda mechi zote watakazocheza nyumbani itaanza rasmi leo.

Mpunga alisema ili wafikie malengo ni lazima wahakikishe hawapotezi pointi hata moja wanapocheza nyumbani na kupambana zaidi wanapokwenda ugenini.

Alisema kwao kila mechi ni muhimu na hawataidharau timu yoyote inayoshiriki katika ligi hiyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >